Nipashe
Ijumaa Mei 29, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580244
www.ippmedia.com
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



# Mama mbaroni madai ya kuua mwanawe na kumzika

UK. 3


Serikali inayopambana kuweka juu mafuta ya michikichi ivuke Kigoma

BUFE

Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ubia wa REA unaposhikamana na Wakala Misitu kuwasha umeme

BIASHARA

UN SUDAN KUSINI...

'Dogo' aliyekombolewa vitani alivyoibuka seremala maarufu

• Kutoka kundi la maelfu waliokuwa msituni

UKURASA 11

# Mwongozo corona kwa wanafunzi, wanavyuo

**WIZARA** ya Afya yatoa mambo manne muhimu ya kuzingatiwa... *Endelea UK. 2*



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu

# Ndalichako azuia wanafunzi kwenda na limao, tangawizi

UK. 2

## BAA LA CORONA



Usimpulizie dawa mtu (akiwa kwenye chumba) haishauriwi kwa vyovyote vile. Njia hii inaweza kumwathiri mtu kimwili na kisaikolojia na haitazuia maambukizo kwa mtu ambaye ana virusi vya corona kupitia majimaji atakayotoa kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## MAPYA YA MCHUNGAJI ANAYEDAIWA KUMPA MIMBA MWANAFUNZI

UKURASA 8




MICHEZO MSOLLA AIPELEKA YANGA HISPANIA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Ndalichako azuia wanafunzi kwenda na limao, tangawizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amepiga marufuku wanafunzi kwenda na tangawizi, limao na spiriti pindi shule na vyuo vitakapofunguliwa huku akizikata shule kupika vyakula vitakavyowaongeza vitamini C.

Amesema hatasita kuzifutia usajili shule ambazo zitageuza uwapo wa corona kama kitega uchumi kwa kuongeza malipo ya ziada.

Profesa Ndalichako alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa baada ya baadhi ya shule kutoa maelekezo kwa wanafunzi kwenda na vitu hivyo.

Alisema shule zimeanza kutoa maelekezo tofauti tofauti kwa wanafunzi kwamba waende na lita mbili za spiriti, wengine waende na limao kavu za unga, tangawizi, jambo ambalo linaweza kuamsha magonjwa mengine yakiwamo ya saratani.

"Unakuta shule inatoa maelekezo tofauti wakati suala la virusi vya corona ni suala la kitaalamu, shule na vyuo vizingatie mwongozo uliotolewa na Wizara ya Afya na siyo kila mtu kuja na maelekezo yake.

"Ni marufuku kwenda na spiriti shuleni, kwanza inaweza kuwaka moto na kuunguza mabweni na ni kilevi, mtu anaweza kutumia, hivyo ni marufuku," aliagiza.

Profesa Ndalichako alisisitiza wazazi kuwapatia barakoa za kitambaa ambazo wanafunzi watazifua na kupiga pasi.

"Wanafunzi wazingatie umbali kati ya mtu na mtu na wajiepushe kusongamana katika majadiliano darasani au bweni, wazingatie taratibu za Wizara ya Afya.

"Wanafunzi wanaenda kuendelea walipoachia kwa fedha zilezile, hakuna malipo ya ziada, nikemee shule ambazo zinataka kutumia corona kama kitega uchumi," alionya.

Profesa Ndalichako alisema kila wakati serikali imekuwa ikitoa maelekezo kwa watu wanaoendesha shule na wanatoa mafunzo kwa Watanzania kuacha roho ya kukomoana.

"Unakuta mtu anasema mwanafunzi aje na kilo moja ya limao ya unga, mimi mwenyewe hata sijui upatikanaji wake, vitu vingine vinatengeneza hofu, tangawizi kilo moja ya unga anaitoa wapi? Mtu anakwenda kukaa shuleni mwezi mmoja na nusu, hiyo yote ya nini?" Alihoji.

Alisisitiza shule kuwapatia wanafunzi vyakula vyenye vitamin C na kuacha kuwatuma wanafunzi vitu vya kutengeneza.

"Kuwapo na maji yanayotiririka ili kunawa na sabuni, suala la vitakasa mikono ni la ziada, lisiwe la lazima," alionya.



Mwendesha bodaboda akiwa amebeba mzigo wa mihogo na abiria akiwa amesimama katika eneo la Chanika nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari na ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwongozo wanafunzi, wanavyuo

**Na Salome Kitomari**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetoa mwongozo wa udhibiti wa corona kwa shule, vyuo na taasisi za elimu nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na wizara hiyo, na kusainiwa na waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu, ilieleza maeneo manne ambayo ni maandalizi ya mazingira ya taasisi za elimu kabla ya kufunguliwa, ni uchunguzi wa afya, usafiri wa kwenda na kurudi shuleni/chuoni na mazingira ya kujifunzia.

Mwongozo huo umetaka wanafunzi, walimu na wafanyakazi wengine kukaa kwa umbali, ikiwamo kuvaa barakoa na kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia sabuni na maji yanayotiririka.

**MARUFUKU SPIRIT**

Wizara imepiga marufuku matumizi ya 'spirit' shuleni au vyuoni na kutakiwa kufuatilia kwa karibu suala hilo.

Mwongozo huo umeeleza kuwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wanafunzi, walimu, watumishi wenye magonjwa ya moyo, selimundu na wenye magonjwa ya mfumo wa hewa kama vile pumu kutokuvaa barakoa.

Pia, wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapaswa kuvaa barakoa maalum zitakazoruhusu mwanafunzi mwenye matatizo ya usikivu kuwasiliana na mwalimu.

Mwongozo huo umeelekeza kutakasa mazingira yote ya shule, chuo au taasisi kwa kuzingatia miongozo ya utakasaji iliyotolewa na Wizara ya Afya, kwa taasisi zinazokuwa zinatunza washukiwa au wagonjwa wa corona.

"Utakasajii huu ufanyike angalau saa 72 kabla ya wanafunzi kuingia. Siku ya kwanza ya kufunguliwa ni muhimu itumike kutoa elimu kwa wanafunzi/wanachuo na wafanyakazi wote kuhusu ugonjwa wa corona pamoja na dalili zake na hatua za kuchukua ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huu," alisema.

**KUNAWA MIKONO**

Maelekezo mengine ni kuhakikisha uwapo wa vifaa vya kunawia mikono (sabuni na maji tiririka) kwa ajili ya usafi wa mikono katika kila eneo au maeneo ya madarasa, ofisi, kila geti/lango kuu, mabweni, maktaba, bwalo la chakula, vyoo na maeneo mengine muhimu.

"Wizara inasisitiza matumizi ya sabuni na maji tiririka ndiyo iwe njia kuu ya usafi wa mikono. Vilevile vifaa vya kunawa mikono vizingatie mahitaji ya wanafunzi/wanavyuo wenye ulemavu. Vitakasa mikono vinaweza kutumika kama mbadala wa maji tiririka na sabuni,"alisema.

Pia, uongozi wa shule/chuo uhakikishe vitakasa mikono vinavyotumika vina ubora unaotakiwa iliyotengenezwa kwa 'ethanol' yenye asilimia zaidi ya 70 kwa wanafunzi na wanavyuo, na kwamba ni suala la hiyari.

"Shule, chuo au taasisi yenye vituo vya kutolea huduma za afya, watumishi wote wanaohusika wapewe elimu juu ya kuwahudumiwa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wote watakaoshukiwa kuwa na corona ikiwamo kuwapatia msaada wa kisaikolojia na kuondoa unyanyapaa," alisema.

Vile vile, alisema shule na taasisi hizo zinapaswa kuwa na dawa na vifaa kwa ajili ya dharura.

Kwa upande wa shule za bweni, wahakikishe kuwapo nafasi ya kutosha kati ya kitanda kimoja hadi kingine na kudhibiti uchangiaji vifaa kwa wanafunzi kama vile taulo, mashuka, vyombo vya kuogea na vifaa vya usafi wa mwili.

Pia, wanafunzi, walimu na wafanyakazi wametakiwa kuvaa barakoa za vitambaa, ikiwamo wazazi na walezi kuwanunulia watoto wao.

**BARAKOA**

Mwongozo huo umetaka uwapo wa utaratibu mzuri wa upatikanaji wa barakoa za vitambaa zinazotengenezwa nchini na ambazo vinaweza kufuliwa na kupigwa pasi kila siku katika maeneo yao kwa gharama nafuu.

"Barakoa za vitambaa vya pamba zenye safu mbili ndizo zinazoshauriwa kuvaliwa kwa kuwa ni bora na salama kiafya. Wazazi wanaweza kuwapa au kuwanunulia watoto wao,"alibainisha.

Pia, taasisi na shule hizo zimetakiwa kuhakikisha uwapo wa vifaa vya kuhifadhia taka zitokanazo na barakoa zilizotumika na kuziteketeza kama taka nyingine hatarishi ili kuzuia maambukizo ya virusi vya corona.

Kuhusu uchunguzi wa afya, alisema iwapo mwanafunzi watahisiwa wapimwe kabla ya kurudi shuleni na watakaobainika wabaki nyumbani hadi hali zao zitakapoimarika, na watakaougua wakiwa shuleni wafikishwe kwenye vituo vya afya vya karibu.

**USAFIRI**

Kwa upande wa usafiri, wamiliki wa magari ya shule/chuo waweke vitakasa mikono kwenye magari yao kwa ajili ya wanafunzi wakati wa kupanda kuelekea shuleni/chuoni, ikiwamo kuvaa barakoa kabla ya kupanda.

Corona iliripotiwa nchini kwa mara ya kwanza Machi 16, mwaka huu, na hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwamo kufunga shule zote za awali, msingi na sekondari, vyuo na taasisi za elimu nchini.

Mei mwaka huu, Rais alitangaza kufungua vyuo, taasisi za elimu nchini na kidato cha sita pamoja na michezo mbalimbali kuanzia Juni mosi, mwaka huu.

## HABARI KITAIFA




Mtumishi wa gari la Shule ya Sun Academy Iringa, Patrick Ng'oka, akipiga debe kuita abiria katika kituo cha daladala cha Makosa, mjini Iringa juzi. Wamiliki wengi wa shule wamelazimika kugeuza mabasi ya wanafunzi kuwa daladala kwa kipindi hiki ambacho shule zimefungwa kutokana na janga la corona. **PICHA: FRANCIS GODWIN** .

# Hukumu leo kuamua Zitto kwenda jela au la

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, anayekabiliwa na kesi uchochezi kuachiwa huru ama kwenda jela itajulikana leo itakaposomwa hukumu yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Mahakama hiyo iliyoketi jana chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, ilipanga kusoma hukumu dhidi ya Zitto leo.

Awali, upande wa Jamhuri katika kesi hiyo uliita mashahidi 15 na utetezi wanane.

Katika kesi ya msingi, Zitto anadaiwa Oktoba 28, 2018 akiwa katika mkutano na waandishi wa habari, uliyofanyika katika makao makuu ya ofisi ya Chama cha ACT -Wazalendo, alitoa maneno ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alinukuliwa "...watu ambao walikuwa ni majeruhi katika tukio la mapambano baina ya wananchi na polisi wakiwa wamekwenda hospitali kupata matibabu katika kituo cha afya Nguruka, polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitali kituo cha afya Nguruka kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua..."

Katika shitaka ya pili ilidaiwa Oktoba 28, 2019 eneo la Kijitonyama katika makao makuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam, alitoa maneno ya uchochezi dhidi ya Jeshi la Polisi akisema "...lakini tumefuatilia kwa kina jambo hili, taarifa ambazo tumezipata kutoka kijijini Mpeta-Nguruka, Uvinza ni mbaya, ni taarifa ambazo zinaonyesha wananchi wengi sana wameuawa na jeshi la Polisi pamoja na kwamba afande Sirro amekwenda kule, haijatoa taarifa yoyote kuhusu wananchi...kama hawa Wanyantuzu walivamia eneo la Ranchi kuna taratibu za kisheria za kuchukua na sio kuwauwa, wananchi wengi sana wamekufa..."

Ilidaiwa kuwa katika tarehe hiyo hiyo, Zitto alitoa maneno ya uchochezi dhidi ya Jeshi la Polisi akisema "... Tumekuwa tukifuatilia kwa kina yanayojiri yote huko Uvinza tunasikitika kusema kuwa taarifa tunazozipata kutoka Uvinza zinaogofya mno, kwani tunaambiwa kuwa wananchi zaidi ya 100 wa kabila la Wanyantuzu wamepoteza maisha kwa kupigwa risasi na polisi, wengine wakisema kuuawa hata wakiwa kwenye matibabu hospitalini baada ya kujeruhiwa kwenye purukushani na jeshi la polisi..."

# Adaiwa kumuua mtoto wake na kumzika

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Kijiji cha Sekedidi, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, Lucia Mahazi (42), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuua mtoto wake wa kiume wa siku mbili na kisha kumzika, kwa madai ya kutelekezwa na mwanamume aliyempa ujauzito.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema tukio hilo limetokea Mei 26, mwaka huu, majira ya saa 12 jioni.

Alisema wananchi wa eneo hilo waligundua kuwa mwananke huyo hakuwa na mtoto aliyejifungua Aprili 17, mwaka huu na kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ambalo lilianza kumchunguza na kubaini mtoto huyo alishauawa na mama yake.

"Uchunguzi wa awali ulibaini mama huyo alijifungua mtoto huyo April 17 na kumuua April 19, na kisha kumzika mwenyewe katika eneo la shule ya msingi Ididi wilayani Kishapu, majira ya saa 12 jioni wakati mvua kubwa ikinyesha ili watu wasimuone," alisema Magiligimba.

"Mabaki ya mwili wa marehemu tumeyatoa Mei 26, kaburini na yamekabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi, na mtuhumiwa yupo chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi," aliongeza.

Vile vile, alisema chanzo cha mauaji ya mtoto huyo, ni mtuhumiwa kudai alikabiliwa na ugumu wa maisha, baada ya mwanaume aliyempatia ujauzito kumtelekeza.

**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**

**KUFUNGULIWA KWA CHUO NA KUANZA KWA MASOMO**

Wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere mnataarifiwa kuwa chuo kitafunguliwa na kuanza masomo Jumatatu tarehe 01 Juni 2020 kwa programu zote na katika kampasi zote.

Wanafunzi wanaokaa kwenye mabweni ya chuo wataanza kuingia kwenye vyumba vyao kama walivyokuwa wamepangwa awali kuanzia Jumamosi, tarehe 30 Mei 2020.

Wanafunzi mnajulishwa kuwa usajili utafanyika kuanzia tarehe 30 Mei 2020 hadi 15 Juni 2020. Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kuingia chuoni baada ya tarehe 15 Juni 2020 kama hajakamilisha usajili.

Wanafunzi wanakumbushwa kuangalia mikondo (streams) na ratiba za masomo kupitia kwenye tovuti ya Chuo. Ratiba hizo zina mabadiliko ambayo yamelenga kupunguza msongamano darasani, na kupunguza uwepo wa wanafunzi wengi chuoni kwa wakati mmoja. Ili kupunguza msongamano usio wa lazima, mwanafunzi asiye na masomo siku husika anashauriwa kutokuwepo eneo la chuo.

Chuo kinawahimiza wanafunzi wote kuzingatia maelekezo yote ya Serikali kuhusu udhibiti wa kuenea kwa ugonjwa wa COVID-19

IMETOLEWA NA

**MKUU WA CHUO**
26 Mei, 2020

157554



**Bonite Bottlers Ltd** inayo furaha kuwaletea **Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa LITA 6, LITA 12 na LITA 18.9.** Tumewekeza katika mitambo ya kisasa ya kuzalisha maji katika ujazo mkubwa ili kuwawezesha wateja, wanywaji na wadau wetu kupata maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na kwenye taasisi mbalimbali.

**UPATIKANAJI:-**

- Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, maduka na wauzaji wa jumla nchi nzima.
- Kwa Wateja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, unaweza kununua maji ya kunywa ya Kilimanjaro ukiwa nyumbani kwa njia ya mtandao kupitia makampuni ya usambazaji bidhaa tunayoshirikiana nayo ambayo ni **Shoponline Tanzania www.shoponline.co.tz** na Piki Deliveries **www.piki.co.tz** .

Ni matumaini yetu mtaendelea kutuunga mkono kwa kuburudika na maji kutoka kilele cha Afrika.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar:** +255 754635988 au +255 22 700450/655, **Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

**MAJI YA KUNYWA YA KILIMANJARO NI MAJI YA KUAMINIKA KILA SIKU!**

# SADC: Usafirishaji bidhaa uendelee licha ya corona

**Na Mwandishi Wetu**

MAOFISA waandamizi na makatibu wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), wamependekeza kuruhusu biashara za bidhaa zote kuendelea kusafirishwa katika nchi zao kama ilivyokuwa kabla ya janga la virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kufungua mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC kwa ngazi ya makatibu wakuu uliofanyika kwa njia ya mtandao juzi jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, alisema mkutano huo umejadili na kutoa mapendekezo ya kuondoa vikwazo vyote vya kibiashara ili kuendeleza uchumi ndani ya jumuiya.

Balozi Ibuge ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Makatibu Wakuu, alisema kuwa uamuzi huo utawawezesha wananchi kuendelea na maisha yao ya kawaida na biashara zao kwa kuwa janga la corona litaendelea kuwapo kwa muda ambao ukomo wake haujulikani japo juhudi za kuukabili ugonjwa huo zinaendelea.

"Kikao cha makatibu wakuu cha leo (juzi), kimependekeza kuondoa kikwazo cha bidhaa mahususi tu kupita katika mipaka yetu badala yake bidhaa zote zinazowezesha wananchi wetu kuendelea na maisha, ni lazima ziruhusiwe kupita katika mipaka ya nchi wanachama wa SADC," alisema.

Katibu Mkuu huyo aliongeza kuwa ni muhimu wa wanaSADC kujumuika katika wakati huu na kuona ni jinsi gani wanaweza kushirikiana na kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi wanachama wa SADC unakua kwa kuongeza juhudi katika sekta ya biashara.

Balozi Ibuge alifafanua: Kwa mfano halisi sisi kama Tanzania hatukufunga mipaka yetu, na katika kutokufunga mipaka yetu, bado tunatambua kwamba tunaendelea kuwategemea wenzetu kama wanavyotutegemea sisi.

"Tuna bandari inayohudumia nchi nane za SADC na zisizokuwa za SADC na ambazo ndizo hasa tunapozungumzia utengamano na mazingiara ya kufanya biashara na kuzingatia tahadhari mbalimbali za uonjwa wa Covid-19 ambazo nchi hizo zimekuwa zikichukua."

Alisema mkutano huo pia ulijadili hali ya kifedha ndani ya jumuiya, utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na kikao cha Baraza la Mawaziri wa SADC ambayo ni menejimenti ya maafa, utekelezaji wa kaulimbiu ya Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC isemayo 'Mazingira Wezeshi kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya Viwanda, Kukuza Biashara na Ajira Ndani ya SADC' na mapitio ya hali halisi ya biashara baina ya nchi.

Alisema viongozi hao pia walijadili maendeleo ya viwanda ndani ya jumuiya na taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Jumuiya na mpango kazi wake.

Mkutano huo ulihusisha wataalamu kutoka nchi wanachama 12 wa SADC kutoka sekta za mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki, fedha na mipango, uchukuzi na mawasiliano, viwanda na biashara, maliasili na utalii pamoja na afya.




Mkurugenzi wa Holt Dream Center, Park Jieun (kushoto), akimkabidhi bima ya afya kutoka Shirika la Holt Dream kwa kushirikiana na Women in Social (WISE) mtoto Samson Tendega akiwa na bibi yake Mekolina Nyakunga, jijini Dar es Salaam jana, ambapo watoto 90 watanufaika na bima hiyo. Wa (pili kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wise, Dk. Astronaut Bagile. **PICHA: MIRAJI MSALADULA.**

# Sababu ushahidi kesi ya Shamim, mumewe kukwama kuendelea

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama Mafisadi imeshindwa kuendelea kusikiliza ushahidi baada ya upande wa Jamhuri katika kesi hiyo kudai kuwa shahidi wao ni mgonjwa.

Kesi hiyo namba 4/2020 inawakabili Abdul Nsembo (45) na mke wake Shamimu Mwasha (41), imepangwa kuendelea leo mahakamani hapo.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Elinaza Luvanda, imeagiza mawakili wa pande zote mbili kuwasiliana kabla ya kufika mahakamani ili kupunguza usumbufu wa kusitisha kazi nyingine wakati kesi haiwezi kuendelea kusikilizwa.

Awali, Wakili wa Serikali, Constantine Kakula, alidai kuwa shahidi waliyekuwa wanamtegemea ameshindwa kufika mahakamani kwa sababu ni mgonjwa, hivyo aliomba kesi hiyo kuendelea leo.

Wakili wa utetezi, Nassoro Juma, alidai kuwa ili kesi iweze kuendelea kama ilivyopangwa, Jamhuri waite mashahidi zaidi ya mmoja ikitokea mwingine ana dharura kesi iweze kusikilizwa.

Jaji alisema ili kuepusha usumbufu, mawakili pande zote mbili wawasiliane na Msajili ili kuondoa usumbufu pale anapokosekana shahidi.

Alisema kesi hiyo itaendelea leo kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kusafirisha dawa hizo za kulevya, Mei mosi, mwaka jana wakiwa eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, kinyume na sheria ya uhujumu uchumi.

# Miaka saba jela kwa kujeruhi mwanawe

**Na Stevie Chindiye,** Tunduru

MAHAKAMA ya Wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma, imemhukumu Mohammed Masud (30), mkazi wa Kijiji cha Mnazi Mmoja wilayani humo kutumikia adhabu ya miaka saba jela baada ya kupatikana na hatia ya kujemruhi mtoto wake.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Honorius Kando, baada ya mshitakiwa kukiri kufanya kosa hilo.

Hakimu Kando alisema mahakama yake imechukua uamuzi wa kumhukumu kifungo hicho baada ya mtuhumiwa kukiri kufanya kosa kwa kumchoma moto aliouwasha kwa kutumia kuni katika miguu yake na kumsababishia ulemavu wa muda.

Alisema kitendo kilichofanywa na mzazi huyo ni ukatili uliopindukia, hivyo adhabu hiyo ni fundisho kwake na watu wengine ambao wamekuwa na tabia za kufanya vitendo vya aina hiyo.

Awali, akimsomea mashtaka hayo ya jinai namba 163/2020, Mwendesha Mashtaka ambaye pia ni Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Stephen Msongaleli, alidai kuwa, katika tukio hilo, mtuhumiwa huyo alimchoma moto na kumsababishia maumivu makali na majeraha katika vikanyagio vya mguu mtoto wake mwenye umri wa miaka saba(jina tunalihifadhi).

Inspekta Msongaleli alidai kuwa hilo ni kosa la kwanza kutekelezwa na mtuhumiwa huyo, lakini aliiomba mahakama kumpatia adhabu kali ili liwe fundisho kwa watu wengine ambao wamekuwa na tabia za kutesa watoto katika jamii.

Alidai taarifa zilizotolewa na maofisa tabibu wa hospitali ya serikali ya Wilaya ya Tunduru anakotibiwa majeruhi huyo, zinabainisha kuwa hadi sasa, mtoto huyo hawezi kutembea kwa kutumia miguu yake jambo ambalo halikubaliki.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Rehema Nyanda, alidai mahakamani kuwa mtoto huyo aligundulika kufanyiwa ukatili huo Machi 15 mwaka huu baada ya majirani kutoa taarifa za kupotea kwa mtoto huyo.

Nyanza aliiomba mahakama hiyo kutoa maelekezo ya mtoto huyo kupelekwa kwa mama yake mzazi mkoani Lindi ili kuepuka vitendo hivyo vya ukatili.

Akijitetea kabla ya hukumu hiyo, Masud aliomba mahakama hiyo kumwachia huru kwa madai kuwa katika tukio hilo alikuwa anamwadhibu mtoto wake baada ya kutuhumiwa na majirani zake kuwa amekuwa na tabia za udokozi.

HABARI KITAIFA

# W/biashara Ufaransa wapiga jeki vita ya gonjwa corona

**Na Faustine Feliciane**

WAFANYABIASHARA wa kifaransa wanaofanya shughuli zao na kampuni yao nchini, wamekabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vya afya kupambana na janga la corona.

Msaada huo waliukabidhi kwa Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier naye kukabidhi kwa mratibu wa mipango wa taasisi ya ' Medicine du Monde" (MdM), Kessy Ndenego mbele ya mwakilishi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Francis Lukuwi.

Kampuni hizo zilizowakilishwa na kampuni sita zilizotoa vifaa mbalimbali vya kupambana na corona kwa wafanyakazi wa sekta ya afya pamoja na kutoa mafuta kwa ajili ya magari yanayotumiwa na sekta hiyo kwenye kuhudumia wagonjwa.

Vifaa hivyo ambavyo havikutajwa thamani yake, vimenunuliwa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na ni sehemu ya ahadi ya Balozi Clavier aliyoitoa Aprili 20, mwaka huu kuwa kampuni za kifaransa nchini zitachangia juhudi za serikali kupambana na janga la corona.

"Janga hili la corona limeathiri kila eneo katika jamii zetu, sote tunapambana kuona namna gani tutasaidiana kupambana nalo, Ufansa ni nchi ya pili duniani kwa kuchangia mapambano haya," alisema Balozi Clavier.

Rais wa mtandao wa wafanyabiashara wa kifaransa nchini (CCEF), Christopher Darmois, kwa niaba ya kampuni zilizotoa msaada huyo, alisema Ufaransa wanayo nia ya kupambana na janga la corona kwa kusaidia mapambano yake na ndio sababu ya wafanyabiashara hao kutoa msaada huo ikiwa ni kuunga juhudi za Serikali kupambana na corona.

"Hakuna jitihada kubwa au ndogo katika mapambano haya na ndio maana tunajitahidi kupambana kusaidia pale tunapoweza,"alisema Darmois.

Mwakilishiwa Wizara la Afya, Francis Lukuwi, alishukuru jitihada hizo za kuungana na Serikali kupambana na janga la corona.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri (kushoto), akikabidhi awamu ya pili ya vitambulisho vya wajasiriamali wadogo 2,000 kwa Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Boniface Magiri, katika hafla iliyofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: TIGANYA VINCENT** .

# Wajasiriamali 59,000 wapewa vitambulisho

**NA Tiganya Vincent**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amekabidhi vitambulisho 59,500 vya awamu ya pili kwa ajili ya wajasiriamali wadogo.

Kutolewa kwa vitambulisho hivyo kunafanya Mkoa wa Tabora kufikisha jumla ya vitambulisho 71,500 vilivyokwishapokewa baada ya awali ya kwanza kupata 12,000.

Vitambulisho hivyo vilikabidhiwa jana na Mwanri kwa wakuu wa wilaya zote za Mkoa wa Tabora ili kuwagawia wajasiriamali ambao sifa zao zinakidhi kupewa vitambulisho hivyo.

Alibainisha kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imepata vitambulisho 7,500, Nzega Mji 10,000, Uyui 10,000 na Manispaa ya Tabora 10,000.

Mwanri alitaja Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imepata vitambulisho 10,000, Sikonge 2,000 Urambo 5,000 na Kaliua 5,000.

Aliwataka wakuu wa wilaya kushirikiana na watendaji katika kuhakikisha vitambulisho vyote vilivyotolewa kwenye awamu ya kwanza vinamalizika mapema.

Awali, Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Tabora, Thomas Masese, alisema ukomo wa vitambulisho hivyo utakuwa Desemba mwaka huu.

Masese alisema ugawaji wa vitambulisho hivyo unatokana na mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mwaka 2015.

Alisema vitambulisho vya sasa ni tofauti na vilivyopita na ugawaji wake kwa walengwa ni lazima kuingiza kumbukumbu muhimu ili kuepuka udanganyifu.

Masese aliongeza kuwa watawafanyia tathmini waliopita kama wana sifa za kuendelea kupata vitambulisho kabla ya kuwapa.

AGRIBUSINESS INNOVATION CENTER AIC TANZANIA

PASS PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

VITUO ATAMIZI VYA KILIMOBIASHARA VYA AIC TANGAZO KWA VIJANA FURSA YA KUJIUNGA 2020/21

Kituo cha Ubunifu wa Kilimobiashara (AIC), ambacho ni idara ya Taasisi ya PASS inapenda kuwatangazia vijana wenye nia ya kufanya kilimobiashara kwamba kinapokea maombi ya kujiunga na Vituo Atamizi vya Kilimobiashara vilivyopo SUA Morogoro na TALIRI Farm, Mbande, Kongwa mkoani Dodoma.

Katika vituo hivi, AIC inawapa fursa vijana ya kuanzisha, kumiliki na kuendesha kilimobiashara kwenye sekta ndogo ya mboga na matunda na mifugo na nyama.

Kijana atakayeomba nafasi hii anatakiwa awe na tabia njema, mtiifu, mwenye nidhamu, mchapakazi, fikra chanya, mwaminifu na anayependa kuona matokeo chanya. Vijana wa Kike watapewa Kipaumbele.

Vijana washiriki kwenye Vituo Atamizi watapewa vifaa, miundo mbinu, na mtaji wa kufanya kilimobiashara ambapo watausimamia kwa kipindi cha miezi 12.

Katika kipindi chote, waatainiwa watapewa usimamizi wa karibu ikiwemo ushauri wa kibiashara na upelembaji, ili kuhakikisha wanafanikiwa katika shughuli zao za kilimobiashara.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, vijana watakaofanikiwa kwenye kilimobiashara, AIC itawawezesha kufanikisha kuanzisha biashara kama hiyo kwenye maeneo yao.

Vijana wenye nia wanashauriwa kutuma maombi yao ya kujiunga na kituo Atamizi kimojawapo kati ya SUA-AIC Morogoro kinachojihusisha na kilimobiashara cha mboga na matunda au AIC Kongwa kilichopo Taliri Farm (PRC), Mbande, Kongwa kinachojihusisha na biashara ya unenepeshaji/ufugaji mbuzi na usindikaji wa nyama ya mbuzi. Vijana 280 watachaguliwa kwenye awamu ya kwanza ya mchujo (200 kwa kituo cha Morogoro na 80 kwa Kituo cha Kongwa) na kati ya hawa, vijana 140 (100 Morogoro and 40 Kongwa) watachaguliwa kwenye awamu ya pili ya mchujo kujiunga na Vituo Atamizi kuanzia Oktoba 2020.

Kwa maelezo zaidi na jinsi ya kupata, kujaza na kurudisha fomu ya maombi yanapatikana kwenye tovuti ya www.aic.co.tz na www.pass.or.tz, SUA-SAEBS, ofisi za AIC (SUA, Morogoro na Mbande, Kongwa) na ofisi zote za PASS nchini.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19/06/2020 saa 11.00 jioni.

157559

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vyama vikubaliane maadili ya uchaguzi

**MOJA** ya mambo muhimu na ya msingi katika mchakato wa uchaguzi mkuu ni maadili, ambayo kuridhiwa na kusainiwa na vyama vyote kabla ya kupulizwa kipyenga.

Tanzania ikiwa ni moja ya nchi zinazojinasibu na kuheshimu uchaguzi huru na haki, inaingia katika mchakato huo, ambao utachukua miezi kadha kabla ya Oktoba mwaka huu.

Uchaguzi huo ni wa madiwani, wabunge na rais, ambapo kampeni za vyama vya siasi zitafanyika kwa ajili ya kuwashawishi wananchi kuvipigia kura wagombea wao.

Maadili hayo huwekwa na kurejelewa kila mwaka wa uchaguzi, na mwaka huu vyama vimepewa nakala ana kuitwa kuyajadili, kusaini kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Ndani ya maadili hayo mambo yanayotajwa ni wagombea au wafuasi wa vyama hivyo kuchana mabango ya wagombea wengine, kutoa lugha chafu wakati wa mikutano ya kampeni pamoja na kupitisha muda wa kufanya mikutano ya kampeni.

Iwapo chama au mgombea atavunja maadili hayo, zipo kamati za maadili za kata na jimbo ambazo zinawajibu wa kuchukulia hatua kali ndani ya saa 48.

Ndani ya maadili hayo adhabu zilizotajwa kwa chama au mgombea ni kuomba radhi wananchi hadharani, kutotumia vyombo vya habari kwa muda flani, onyo la maandishi, kusimamishwa kufanya kampeni, mgombea kutangaza mbele ya vyombo vya habari kuwa yeye ni bingwa wa kuvunja maadili ya uchaguzi au kutozwa faini Sh. 100,000.

Aidha, maadili hayo yanataka chama cha siasa ambacho kinataka kufanya mabadiliko ya ratiba ya mikutano ya kampeni, lazima kimfahamishe msimamizi wa uchaguzi wa kata na ombi hilo lazima lijadiliwe na vyama vyote vinavyoshiriki kwenye uchaguzi.

Juzi Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), iliviita vyama vya siasa kujadili na kupitisha maadili ya uchaguzi kwa mwaka 2020, ambao walitakiwa kufanya hivyo kwa siku moja.

Katika kikao hicho, Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kililalamikia kutengwa kwa muda huo kwa kuwa hautoshi kusoma, kujadili na kufanya marekobisho.

Kwamba sheria ilivyo imeweka kwenye maadili hayo kifungu ambacho kinavilazimisha vyama kama kama hayapo sawasawa lazima wasaini.

Kilidai ni kitu ambacho hakikubaliki, lakini kwa kuwa wamshakiweka wanalazimika kusaini na baadaye watawasilisha marekebisho yao.

Baadhi ya vyama pia vilieleza kasoro kadhaa, hivyo, inawezekana kukawapo na upungufu kadhaa katika mchakato huo, ambayo yanahitaji kutatuliwa kabla.

Tunaona kuna haja kwa NEC kusikiliza pande zote; kwa maana wadau wote wa uchaguzi huo ili mchakato kuo uendeshwe katika mazingira rafiki kwa wote.

Jambo la kupongeza ni kuwa NEC imekuwa ikiwashirikisha wadai miaka yote kabla ya uchaguzi kwa ajili ya kipokea maoni na ushauri wao.

Maadili hayo yanabeba utaratibu mzima wa kucheza mchezo wa siasa kuanzia Agosti hadi Oktoba, na ndiyo inajenga msingi imara wa kuonyesha kuwa uchaguzi ni wa huru na haki, hivyo kuondoa shaka kwa baadhi ya wadau.

Tinaishauri NEC kuendelea kiwashirikisha wadai wengine wa uchaguzi ili watoe maoni, ushauri na wasiwasi wao, hatomaye muda wa kusaini maadili hayo kila upande uridhike, na hivyo kutokuwapo malalamiko mchakato wa uchaguzi utakapoanza hususan kampeni.

Ni vyema maadili hayo yakaridhiwa na wadau wote baada ya kuwa na muda wa kutosha kusoma na kupitisha kuliko kuharakisha na kuwaacha wengine wakiwa na malalamiko na hata wakitoa maoni yao hayatafanyiwa kazi, kwa kuwa tayari maadili yatakuwa yameshachapishwa katika Gazeti la Serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Beatrice Moses

# Kidato sita, wanavyuo mcheni Mungu kivitendo vita corona

HATUANGAMII kwa neema ya Mungu tu, wala si kwamba sisi Watanzania ni wajanja sana ikilinganishwa na wenzetu, bali kwa kuamua kumlilia Muumba ametuhurumia.

Ni wazi tunapaswa kuendelea kumuomba na kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya katika kudhibiti maambukizo ya homa kali ya mapafu Covid 19.

Hivi karibuni serikali ilitangaza wanafunzi wa kidato cha sita na vyuo warejee kuendelea na masomo. Ni uamuzi baada ya kufungwa shule na vyuo tangu Machi 17 mwaka huu, hatua inayolenga kudhibiti maambukizo ya ugonjwa unaoendelea kuitikisa dunia.

Ni wakati ambao wanafunzi wa kidato cha sita wanatakiwa kuonyesha uelewa wao kama wasomi, kwa kuzingatia taratibu za kujikinga na maambukizo hayo.

Korona imevuruga ratiba kwenye sekta nyingi, ikiwamo ya elimu. Vijana wa kidato cha sita walipaswa wawe wameshamaliza Mtihani wa Taifa sasa, wakihamia mchakato wa mengine kama vile kusubiri matokeo yao ya mitihani na kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa(JKT), kwa mujibu wa sheria, kwa wale wateule.

Tayari serikali imeshatangaza ratiba mpya ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita, inayotarajiwa kuanza Juni 29 mwaka huu nchini kote na kumalizika Julai 16.

Nachukua fursa hii kuwasisitiza vijana hao, wahakikishe wanaendelea kumuomba Mungu kwa bidii, kama mamlaka za nchi na kiimani, pia wazazi wao wanandeleza.

Vivyo hivyo, pamoja washiriki kikamilifu katika kuzingatia taratibu na miongozo ya kudhibiti maambukizo, ili ratiba zao zikamilike kama ilivyopangwa na kukusudiwa.

Tumeshuhudia vifo vya maelfu na mateso kwa wananchi hadi kwa nchi zilizoendelea kama vile Marekani , China na Italia hali licha ya juhudi kubwa na uwezo wa vifaa na ujuzi wavyotumika kudhibiti maambukizo hayo.

Rais Dk. John Magufuli, kwa kuwa na uhakika na nguvu na Mungu, ndipo alipoamua kuhamasisha wananchi kumuomba muumba huyo kwa bidii zikatengwa siku tatu maalumu za maombi, huku akikataa kuwekea vizuizi (lockdown) kwenye miji hasa Dar es Salaam, kwa kubainisha kuwa ni hatua itakayowazuia wananchi kujitafutia kipato.

Baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa waliinuka na kulaani hatua hiyo ya Rais Magufuli, aliyeamua kuchunguza uwezo wa vipimo vinavyotumika nchini kupima virusi vinavyosababisha ugonjwa huo na matokeo yameshaanikwa.

Ni wakati huu ambao wanafunzi wa kidato cha sita na vyuo wanapaswa kushiriki kikamilifu kudhibiti maambukizo hayo ili kuwezesha serikali kuruhusu wanafunzi wa madarasa ya chini, zikiwamo shule za awali na msingi kurejea darasani.

Miongoni mwa wanavyuo, wapo wanaopenda anasa, hivyo wanajisahaulisha kuwapo kwa ugonjwa huo, hivyo wanaendelea na maisha yao waliyozoea wakitumia uhuru pasopo mipaka waliowekewa, jambo linalohatarisha maisha yao na wengine kwa ujumla.

Baadhi ya wanajamii wamekuwa hawazingatii taratibu zilizowekwa katika kudhibiti ugonjwa huu. Inawezekana hiyo ikasababishwa na uelewa mdogo wa mambo, hasa yanayohusu afya na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Muhimu kila wanafunzi wa kidato cha sita na chuo, ahakikishe barakoa inakuwa miongoni mwa vazi muhimu kwa kila siku, kukumbuka kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka pamoja na kutumia vitakasa mikono (sanitizer).

Uwepo wa corona, umebadili taratibu za maisha, kama vile kusalimiana kwa kushikana mikono. Jamii iepuke kukumbatia na kushikana mikono wakati kuasalimiana marafiki ambao hamjaonana muda mrefu, furahieni kivingine, kukumbatiana marufuku.

Kidato cha sita na wanavyuo, dhihirisheni kuwa ni wacha Mungu na watu makini, kwa kushiriki kikamilifu kudhibiti maambukizo haya, hivyo kuwa mfano kwa jamii na kuonyesha tofauti ya uelewa mambo mlionayo.

HABARI KITAIFA

# Daktari kortini madai rushwa

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Singida imemburuza mahakamani Dk. Abdul Sewando wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Singida (Mandewa), akishtakiwa kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa mgonjwa.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Singida, Adili Elinipenda, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Mei 5, 2020 majira ya saa 9.30 alasiri baada ya kuwekewa mtego na kujiridhisha kuwapo kwa tuhuma hizo.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa na maofisa wa Takukuru baada ya kumaliza kumsafisha mgonjwa akiwa eneo la hospitali hiyo.

Elinipenda alisema awali uchunguzi wa Takukuru mkoani hapo ulibaini, Mei 6, 2020 mtuhumiwa alipokea Sh. 60,000 kutoka kwa mgonjwa ambaye jina lake limehifadhiwa ili ampe huduma ya kumsafisha baada ya kumfanyia vipimo vya 'Ultra Sound'.

Alisema uchunguzi wao pia ulibaini kuwa mtuhumiwa alielekeza atumiwe fedha hizo kwa njia ya mtandao na alizipokea kwa njia ya M-pesa kupitia simu yake.

Alitoa tahadhari kwa watumishi wa idara ya afya mkoani humo kufanyakazi kwa kuzingatia maadili na miiko ya taaluma zao hususani kipindi hiki ambacho jamii inawategemea kutokana na janga la corona.



Gari likipita kwa shida kwenye dimbwi kubwa la maji yaliyotuama kwa muda mrefu na kusababisha usumbufu mkubwa katika maeneo ya viwandani Keko, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**.

# Wataka mpunga uuzwe kwa stakabadhi ghalani

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKULIMA wa mpunga katika Kijiji cha Nyanembe, Kata ya Kilango Halmashauri ya Mji wa Kahama, wameiomba serikali kupitia Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), kuingiza na kuuza zao hilo kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani kama ilivyo kwa korosho na dengu.

Waliyasema hayo jana wakati wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wakiwa kwenye mashamba yao wakiendelea na mavuno ya zao hilo walisema, wakilalamika kuwa wanunuzi wa mpunga wanawalazimisha kutumia vipimo hivyo ambayo vingi vinamnyonya mkulima kwa kuwa na ujazo mkubwa.

Musa Bundala, alisema endapo zao hilo likiingizwa katika mfumo wa stakabadhi gahalami, wakulima wataondokana na ulanguzi wa mazao unaofanywa na madalali hususani katika kipindi hiki cha uvunaji kwa kuwa sheria zitawazuia wanunuzi kwenda moja kwa moja shambani kwa mkulima.

Shika Madaha, alisema wakulima wengi wanazalisha mazao ya biashara, upangaji wa bei umekuwa ukifanywa na wanunuzi badala ya wakulima kila mwaka hasa wakati wa mavuno.

"Kwa sasa gunia la debe sita la mpunga linauzwa kwa Sh. 35,000 hadi 40,000, bei ambazo hazimnufaishi mkulima. Walanguzi wanatufuata moja kwa moja hadi shambani kununua mpunga badala ya kusubiria mzigo sokoni," alilalamika.

Mwenyekiti wa (KACU), Emanuel Charahani, akitolea ufafanuzi, alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilishatoa maelekezo kuhusiana na kuyaingiza mazao ya kimkakati katika ushirika na kuanzia msimu wa kilimo wa mwaka 2021/22, zao hilo litanunuliwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

# Dk. Abbas: Corona tumejua unafiki wa dunia

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, amesema corona imeisaidia Tanzania kuujua unafiki wa dunia, kutokana na hali halisi ya kupambana na ugonjwa huo inavyo endelea duniani.

Aliyasema hayo jana kupitia mahojiano na Televisheni ya Taifa (TBC), kuwa baadhi ya watu walitabiria Afrika kuwa itaathiriwa zaidi na ugonjwa wa corona lakini hali ipo tofauti na matarajio yao.

Alisema wapo watu walioiaminisha dunia kuwa ili kupambana na corona ni lazima kufungia watu ndani na baadhi ya nchi za Afrika zikashawishika kulitekeleza hilo, lakini Tanzania haikutimiza hilo na hali ni nzuri.

"Serikali ilichukua hatua zaidi ya 50 katika kupambana na ugonjwa huu, baadhi ya watu walijaribu kulazimisha nchi za Afrika kufungia watu na hata kukopa fedha wakiamini kuwa hiyo ndio njia pekee ya kupambana na corona," alisema.

Alisema kuna baadhi ya nchi zilifunga hadi nyumba za ibada, lakini Tanzania haijalitekeleza hilo na miongoni mwa sehemu ambazo mpaka sasa zina idadi ndogo ya maambukizo ni Tanzania.

Vile vile, alisisitiza kuwa katika kupambana na ugonjwa wa corona inahitajika ufahamu na sayansi ya hali ya juu kufanya maamuzi ili kuepusha madhara kwa wananchi na Taifa kiujumla.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA AGIZO LA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Februari mwaka huu lilitolewa Agizo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Taasisi zote za Umma, Wizara na Idara za Serikali na wakala za serikali zinazodaiwa malimbikizo ya kodi ya pango na Shirika la Nyumba la Taifa ziwe zimeshalipa madeni yao kabla au ifikapo Mei 30, 2020.

Tunapenda kuzishukuru Taasisi, Idara na Wizara zilizotimiza wajibu wao kwa kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa. Hata hivyo, zipo taasisi kadhaa ambazo hazijatimiza wajibu wao wa kulipa kodi na malimbikizo yao wanayodaiwa na Shirika. Tunapenda kuzihimiza taasisi ambazo hazijatekeleza Agizo la Serikali zijitahidi kulipa madeni yao kabla Shirika halijawasilisha taarifa rasmi ya ulipaji wa madeni kwa Mamlaka kwa hatua stahili.

Lipa kodi yako ili tujenge Taifa letu

LIMETOLEWA NA:

OFISI YA MAWASILIANO KWA UMMA
NA HUDUMA KWA JAMII NHC- MAKAO MAKUU

157535

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (katikati), akikabidhi pikipiki 14 kwa Maofisa Tarafa wa Mkoa huo, mjini Shinyanga jana. **PICHA: ANTHONY ISHENGOMA**.

# Mapya ya mch. anayedaiwa kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Salome Kitomari**

MAPYA yameibuka tukio la Mchungaji wa Kanisa la Mlango wa Ukombozi Gairo, mkoani Morogoro, Joseph Gervas (28), kumtumia kingono binti wa miaka 17 (jina limehifadhiwa) tangu mwaka jana mwishoni.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Morogoro, Wililbrod Mutafungwa, akizungumza na Nipashe, alisema Mchungaji huyo alikuwa akifanya ngono na mwanafunzi huyo wakati mkewe amefasiri au yuko shambani.

Tukio hilo lilitokea wiki iliyopita katika kijiji cha Rubeho Kata ya Kisitwi,Tarafa ya Gairo wilayani Gairo.

Alisema mchungaji huyo alianzisha kituo cha maombi nyumbani kwake, kwamba mwanafunzi huyo alikuwa na tatizo na uoni hafifu, wazazi walishindwa kumnunulia miwani na kuamua kumpeleka kwenye maombi.

"Akiwa kwenye kituo hicho mchungaji akaanza kumuingilia toka mwaka jana wakati mke wa mchungaji akisafiriki au kwenda shamba, huku akimwaminisha ndiyo namna ya kupona tatizo lake," alisema. Mutafungwa alisema binti huyo alipokwenda kwa wazazi wake waliona dalili za ujauzito na walipompima walibaini ana mimba, alivyohojiwa alikiri kuwa na mahusiano ya kingono na Mchungaji huyo.

"Tunamshikilia mchungaji huyo kwa uchunguzi zaidi na kwa usalama wake kwa kuwa huko alikotenda tukio walitaka kumdhuru, tunamhoji kuhusu kituo hicho na upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani siku ya Jumatatu," alisema.

Aidha, uchunguzi na mahojiano kwa wanawake na mabinti wengine unandelea kupitia dawati la jinsia. "Tunawaomba waliokuwa wakihudhuria maombi na kufanyiwa unyanyasaji wowote atoe ushahidi katika hili. Nimemwagiza Mkuu wa Polisi wilaya kwenda kuwahoji watu wote kwa usiri," alisema.

Alisema pia ameagiza kukamatwa na kuhojiwa kwa kiongozi wa kanisa hilo Gairo, ili kujua lengo la kuanzishwa kwa kituo hicho cha maombi huko kijijini na tukio hilo kwa ujumla. Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari, wanapotafuta uponyaji kuwa makini ikiwamo kutambua kama ni suala la kisayansi litibiwe kisayansi wakati wakienda kwenye maombi.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**OFISI ZA TRA KUWA WAZI JUMAMOSI NA JUMAPILI NCHI NZIMA**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa, ofisi za TRA nchi nzima zitakua wazi siku ya **Jumamosi** tarehe **30 Mei, 2020** na **Jumapili** tarehe **31 Mei, 2020** kwa ajili ya kutoa huduma kwa walipakodi kuanzia **saa 2:30 asubuhi** hadi **saa 11:00 jioni.**

**WOTE MNAKARIBISHWA!**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

**Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi**

**TRA MAKAO MAKUU**


# 'Hosteli za Magufuli ziko salama corona'

**Na Romana Mallya**

OFISI ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, imesema Hosteli za Magufuli katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ambazo zilitumika kama karantini kwa washukiwa 844 wa corona, ni salama kwa matumizi kwa wanafunzi.

Kati ya waliokaa kwenye hoteli hizo, 426 ni waliokutana na wenye maambukizo na 418 walikuwa wasafiri waliokuwa wakiingia nchini.

Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Mkoa katika ziara ya viongozi wa chuo waliofika kwenye hosteli hizo zilizopo eneo la Mlimani City, Neema Kweba, alitoa kauli hiyo jana baada ya kukagua usalama wa hosteli hizo.

Waliozuru hosteli hizo ni Mkuu wa chuo hicho, Dk. Jakaya Kikwete (Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne), Makamu Mkuu wa chuo, Prof. William Anangisye, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Jaji mstaafu Damian Lubuva.

Kweba ambaye ni Ofisa Lishe, alisema Hosteli za Magufuli ni salama kwa watu kukaa kwa sababu baada ya washukiwa kuondoka, walizifanyia utakasaji na majengo hayo yamekaa mwezi mmoja yakiwa wazi.

"Yamefanyiwa utakasaji kila chumba, kila kitanda na kila godoro na kila sehemu iliyopo katika majengo haya. Nitoe rai kwa wanafunzi waje bila woga kwa sababu yapo sawa na tuendelee na juhudi za kujikinga kwa kuwa ugonjwa bado upo," alisema.

Alisema majengo hayo yalitumiwa na watu hao kwa muda wa siku 21 zilizoanzia Aprili 5 na mara baada ya kuondoka kama ambavyo Rais John Magufuli alivyoagiza, yalifanyiwa utakasaji.

Alisema Aprili 25, watu wote walioondoka kwenye hosteli hizo na kwamba walipokuwapo walizingatia mambo muhimu ya afya ya kujikinga na kuwakinga waliokuwa wakihudumiwa.

# Mdee ana kesi kujibu tuhuma uchochezi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imesema Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, anayekabiliwa na kesi ya uchochezi ana kesi ya kujibu dhidi ya tuhuma hizo.

Kadhalika, imesema itaanza kusikiliza ushahidi wa utetezi Juni 25 na 26 na mshtakiwa anatarajia kuita mashahidi watano.

Uamuzi huo, ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wao.

Awali, upande wa Jamhuri ulidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kusikiliza uamuzi wa kama mshtakiwa ana kesi ya kujibu au la.

Hakimu Simba alisema, mshtakiwa ana kesi ya kujibu hivyo mahakama yake itaanza kusikiliza ushahidi wa utetezi Juni 25 na 26, mwaka huu.

Mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri wametoa ushahidi akiwamo Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Urafiki, Mrakibu wa Polisi (SP), Batseba Kasanga.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Julai 3, 2017 katika Makao Makuu ya Ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), iliyopo Mtaa wa Ufipa, Wilaya ya Kinondoni, Mdee anadaiwa kutamka maneno dhidi ya Rais John Magufuli kuwa: 'Anaongea ovyo ovyo, anatakiwa afungwe breki' kitendo ambacho kingeweza kusababisha uvunjifu wa amani.

Mdee alifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza na kusomewa mashtaka yake Julai 10, 2017 na yupo nje kwa dhamana.

# 'Marufuku kutozwa faini katikati ya ziwa'

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amesema ni marufuku mvuvi yeyote kutozwa faini katikati ya Ziwa Victoria na atakayebainika kuvunja sheria akamatwe.

Aliyasema hayo alipokuwa akipokea boti tatu zilizonunuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba mkoani Kagera kwa kutumia mapato ya ndani kwa ajili ya kufanyia doria.

Alisema kuwa anapokea malalamiko kutoka kwa wavuvi kuwa wanakamatwa ziwani na kutozwa hela bila kupewa risiti halali na kumuonya ofisa wa serikali anayefanya hivyo anahujumu mapato ya serikali.

"Kwa nini mmalizane katikati ya ziwa, mchukueni huyo mwananchi aliyefanya makosa mpeleke ofisi yoyote ya serikali hata kama ni kisiwani, apigwe faini apate risiti za serikali za kielektroniki, ionyeshwe kwamba alifanya kosa na ameadhibiwa kihalali," alisema.

Alisema anatumia ujumbe wa maandishi na baadhi ya wavuvi wakilalamikia hali hiyo na kuonya kuwa kama ni kweli wahusika waache mara moja maana ikithibitika watawajibishwa.

# RC Pwani ataka usimazi mizani mnada ufuta

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amewaelekeza Wakala wa Vipimo mkoani humo kusimamia ubora wa mizani kwenye minada ya zao la ufuta ili kuzuia wakulima kupunjwa kiwango cha mazao yao.

Amewataka viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika kuhakikisha vifungashio vinapatikana kwa wakati kwa wakulima.

Alitoa maelekezo hayo wakati wa kikao cha wadau wa zao la ufuta kilichofanyika mjini hapa.

Alisema, ili mfumo wa stakabadhi ghalani ambao umeleta ufanisi katika baadhi ya maeneo nchini ikiwamo Wilaya ya Kondoa uwe na tija kwa wakulima wa ufuta wa mkoa huo, ni vyema maelekezo hayo yakafuatwa.

Alielekeza mnada wa ufuta kuratibiwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa kushirikiana na wadau muhimu wa zao hilo, pia wakulima walitakiwa kuongeza uzalishaji na ubora wa zao kwa kuweka mashamba yao katika haki ya usafi na kuepuka kufanya udanganyifu kwa kuchanganya ufuta na mchanga.

Ndikilo alisema, mkoa huo ni kati ya inayozalisha ufuta nchini na katika msimu wa 2019/2020 kilo 7,326,980 zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilion 19 zilizalishwa.




Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (kulia), akimsikiliza Mkuu wa Mauzo Vodacom Tanzania PLC Kanda ya Kaskazini, George Venanty (wa tatu kulia), wakati kampuni hiyo, kupitia asasi yake isiyo ya kiserikali ya Vodacom Foundation walipokabidhi vifaa kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti), vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 42 kwenye Hospitali ya Muriet mkoani humo, juzi, ili kuwapa uwezo wa kupumua, kuongeza joto na kuwapa tiba mwanga. Wa pili kulia ni Mganga Mkuu wa Jiji la Arusha, Dk. Kheri Kagya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Tasaf sasa kulipa walengwa kielektroniki

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), unatarajia kuanza rasmi mwezi ujao utekelezaji wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya mfuko huo, kupitia mfumo mpya wa malipo kwa njia ya kielektroniki kwa walengwa wa kaya zote zinazoishi katika mazingira duni nchi nzima.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga, alisema utekelezaji wa mpango huo kwa kipindi cha pili ulitakiwa uwe umeanza, lakini ulichelewa kutokana na tishio la ugonjwa wa corona.

"Awamu hii ilitakiwa iwe imeanza, lakini imechelewa kutokana na tishio la ugonjwa wa corona, kama ambavyo Rais amesisitiza kwamba watu waendelee kuchapa kazi, tutafanya kazi hii kwa tahadhari kubwa kwa kuzingatia utaalamu unaotolewa na wataalamu wa afya," alisema Mwamanga.

Alisema katika awamu hiyo watatumia kulipa walengwa kwa njia ya kielektroniki kwa kupitia simu zao za mkononi au benki tofauti ya kipindi kilichopita.

"Tasaf ilianza utaratibu wa kulipa ruzuku kwa walengwa kwa njia ya kielektroniki kwa majaribio mwezi Mei 2017 katika halmashauri 16, nchini, hadi kufikia Januari mwaka huu, walengwa 55,539 kati ya 10,299 kwenye halmashauri hizo walikuwa wamejiunga na mfumo huo," alisema Mwamanga na kuongeza:

"Baada ya utekelezaji wa miaka miwili ya majaribio kupitia njia ya kielektroniki, tumebaini kwamba mfumo huo una ufanisi mkubwa, hata kwa upande wa uendeshaji umepunguza gharama za uendeshaji kwa Tasaf, kwa hiyo tumeamua kuutumia nchi nzima kwa sababu tumeona umeleta mageuzi."

Alisema kwa sasa wanafanya kazi ya kutoa elimu na kuhamasisha walengwa wote kujiandikisha katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), ili wapate vitambulisho na kusajili laini zao ambazo zitatumika kupokea fedha zao au kufungua akaunti benki.

# Ofisa mapato matatani madai ya utoro kazini

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Rehema Saidi Bwasi, kumsimamisha kazi mara moja Ofisa Mapato wa Halmashauri hiyo kutokana na utoro kazini na kutohudhuria kikao cha Baraza Maalum la Madiwani kilichotakiwa kufanyika Mei 26, mwaka huu na baadaye kuahirishwa.

Alitoa agizo hilo juzi mwanzoni mwa kikao cha Baraza Maalum la Madiwani la Halmashauri ya wilaya hiyo kilicholenga kujadili taarifa na majibu ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Akiwa anaendelea na kikao hicho, alitaka kujiridhisha iwapo wakuu wa idara wote na vitengo wameshiriki kikao hicho muhimu kama ilivyokuwa imeelekezwa siku chache kabla ya kikao hicho.

Hata hivyo, ilibainika kutokuwapo kwa Ofisa Mapato huyo, Charles Komba na kibali alichokuwa amekiomba kusafiri tangu siku ya kikao hicho kilikuwa hakijapitishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo huku yeye akiwa tayari hayupo kazini.

Mkuu huyo wa mkoa alilazimika kumuuliza mkuu wake wa Idara ya Uhasibu kuhusu mtumishi huyo kutokuwapo kazini, ambaye alimueleza kuwa ni kweli mtumishi huyo aliomba ruhusa, lakini hakuruhusiwa badala yake alitaarifiwa asiondoke, pia alitaarifiwa kushiriki kikao hicho jambo ambalo hakulitekeleza.

Kufuatia maelezo hayo, Sanare alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Rehema Bwasi, kumsimamisha kazi mara moja mtumishi huyo huku akimtaka pia kusimamisha mshahara wake hadi pale suala lake litakapopatiwa ufumbuzi.

"Hapa nikitoka sasa hivi uwe umekwisha mwandikia barua ya kumsimamisha kazi huyo, huko aliko kwa utoro, na usimlipe mpaka jambo lake litakapopatiwa utatuzi," alisema Sanare.

HABARI BUNGENI

# Wanaopaswa kulipa kodi ya zuio watajwa



BUNGE limeelezwa Sheria ya Kodi ya Mapato inamtaka mmiliki wa nyumba ya biashara mwenye mapato yanayozidi Sh. 500,000 kulipa kodi ya zuio (Withholding Tax).

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Fedha na Mipango ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul.

Katika swali lake, mbunge huyo asilimia 10 ya kodi ya pango inapaswa kulipwa na mwenye nyumba za biashara, lakini kwa sasa hulipwa na wapangaji.

"Je, ni lini utaratibu huo utabadilika?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema kwa mujibu wa kifungu cha 86(1)(c) Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, mmiliki huyo anatakiwa kulipa kodi hiyo kutokana na mapato yanayotokana na upangishaji wa pango kwa kiwango cha asilimia 10 ya mapato ya kodi ya pango husika.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, kifungu cha 82(2)(a) mpangaji ambaye sio mfanyabiashara na hajasajiliwa na kama mlipakodi hapaswi kukusanya kodi hiyo.

"Ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi hii, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 inaruhusu mpangaji anayeendesha biashara katika nyumba husika na kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato kuwa wakala wa ukusanyaji wa kodi hiyo," ilisema.

Aidha, ilisema kwa kuwa kodi hiyo siyo ya mpangaji, kiasi cha kodi ya pango ambacho kimelipwa na mpangaji huhesabiwa kama sehemu ya fedha ambazo anapaswa kurejeshewa na mwenye nyumba.

"Utaratibu huu umewekwa ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi hii ya pango kwani inarahisisha kwenye ukusanyaji wa kodi hasa pale ambapo mpangishaji hajasajiliwa na Mamlaka ya Mapato kama mlipakodi," ilifafanua.

# Fursa zaidi zaja elimu ya ufundi






Habari na Augusta Njoji

SERIKALI imesema inaendelea kupanua upatikanaji wa fursa za masomo ya ufundi stadi kwa kujenga vyuo vipya hasa maeneo ya vijijini ambayo hayakuwa nayo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa kauli hiyo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Zubeda Sakuru.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kumekuwapo na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA), lakini wanafunzi waliojiunga na vyuo hivyo hawapati mikopo kutoka serikali.

"Je, serikali itaanza lini kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya ufundi stadi?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema Sheria ya Bodi ya Mikopo (Sura 178) inawabainisha walengwa kuwa ni Watanzania wahitaji walioomba mkopo na wenye sifa za kujiunga na taasisi za elimu ya juu na sio vyuo vya ufundi stadi.

Ilisema serikali imeendelea kutambua kuwepo kwa umuhimu mkubwa wa mafunzo ya ufundi stadi kama kipaumbele chetu cha kujenga uchumi wa viwanda.

"Hivyo serikali imeendelea kubeba gharama nyingi za vyuo vya ufundi stadi vya serikali ambavyo havilengwi na sheria hiyo ili ada zao ziwe nafuu na Watanzania wa kawaida waweze kumudu," ilisema.

Pia, ilisema kwa sasa utaratibu utaendelea kuwa huo huo wa serikali kuvipa vyuo hivyo vya ufundi stadi ruzuku ili kumpunguzia mwananchi wa kawaida gharama za kusoma.

"Hata hivyo, maoni ya Mheshimiwa Zubeda na wadau wengine yanaendelea kupokelewa ili kuboresha utaratibu wa sasa kwa kadri uchumi wetu unavyoendelea kuimarika," ilisema.



# 109 wawekeza viwanda vipya mazao ya kilimo kwa miaka 5

WIZARA ya Kilimo imesema wawekezaji 109 wamewekeza katika uzalishaji wa viwanda vipya vya kuchakata mazao ya kilimo ikiwamo ya chakula kwa kipindi cha miaka mitano.

Hatua hiyo, imeongeza ajira kutoka wastani wa watu 3,880,262 hadi kufikia wastani wa watu 5,204,607.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na wizara hiyo ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Chumbuni (CCM), Ussi Pondeza, ambaye alisema Tanzania inatekeleza sera mbalimbali ili kuwa na uchumi wa viwanda.

"Je, serikali ina mikakati gani ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, matunda na viungo katika kufanikisha sera ya viwanda?" Alihoji.

Pia, alitaka kujua kuna wawekezaji wangapi wa mazao ya vyakula ambao wamejitokeza kuwekeza katika sekta ya kilimo tangu kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa Tanzania kuwa na uchumi wa viwanda.

"Je, serikali imechukua hatua gani katika kuwaondoa wananchi katika kilimo cha asili na kuwaingiza katika kilimo cha kisasa?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema idadi hiyo ni kwa kipindi cha kuanzia 2015/16 hadi 2019/20.

Ilibainisha kuwa serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ili kufanikisha sera ya viwanda nchini.

Ilitaja mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha mfumo wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo kwa kushirikisha sekta ya umma na sekta binafsi.

"Kuendelea kutathmini mahitaji na uwezo wa viwanda na kuviunganisha na wazalishaji wa mazao hayo, kusajili wakulima na wadau wa mazao hayo kwa ajili ya kuratibu uwekezaji na upatikanaji wa huduma na taarifa, kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya Tehama," ilisema.

Mingine ni kuimarisha majadiliano na taasisi za fedha ili kuongeza ugharamiaji katika mnyororo wa thamani wa mazao hayo na kuendelea na majadiliano kati ya serikali na kampuni za bima ili kutekeleza bima ya mazao katika sekta ya kilimo.

"Serikali inatekeleza mikakati ya kuboresha kilimo nchini ili kuwaondoa wakulima katika kilimo cha asili na kulima kwa mfumo wa kisasa," ilisema.

Aidha, ilisema mikakati hiyo ni pamoja na kufanya utafiti wa teknolojia za zana za kilimo katika kulima, kupanda, kuvuna na kusindika na kuhamasisha matumizi ya matrekta badala ya jembe la mkono.

Ilibainisha matrekta makubwa na matrekta ya kukokotwa na mkono yameongezeka kutoka 14,200 na 6,348 mwaka 2015 hadi 18,088 na 8,883 mwaka 2019.

"Mikakati mingine ni kufanya utafiti wa magonjwa na visumbufu vya mimea vinavyoathiri mazao ili kuongeza tija, ubora na uzalishaji wa mazao nchini ambapo kutoka mwaka 2015/16 hadi 2019/20, TARI imegundua aina 124 za mbegu bora," ilisema.

Kadhalika, ilisema kampuni binafsi zimegundua aina 35 za mbegu bora za mazao ya kilimo na jitihada nyingine ni kuongeza matumizi ya mbegu kutoka tani 10,946 hadi 76,725.52 na mbolea kutoka tani 302,482, 2015/16 hadi 604,978 mwaka 2019/20.


Ukurasa 12

Serikali inayopambana kuweka juu mafuta ya michikichi ivuke Kigoma


Ukurasa 13

**Ubia wa REA inaposhikamana na Wakala Misitu kuwasha umeme**



BIASHARA

UN SUDAN KUSINI...

# 'Dogo' aliyekombolewa vitani alivyoibuka seremala maarufu

• Kutoka kundi la maelfu waliokuwa msituni

**Na Mwandishi Wetu**

NCHINI Sudan Kusini kumekuwapo vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa muda mrefu, sasa vikiwa katika hatua ya kupoa. Kuna watoto waliokuwa wakitumikishwa vitani na hatimaye sasa wameachiliwa huru.

Ni hatua inayowafanya kubadili maisha yao na wengine baada ya kupatiwa stadi za kujipatia kipato kwa msaada wa Umoja wa Mataifa na wadau wake, wanaanza kukomboka katika sura ya kuitegemea na wanabadili maisha yao yakiwa na sura ya faraja zaidi.

Miongoni mwa watoto hao ni Malis (si jina lake halisi) ambaye sasa anamiliki karakana ya kutengeneza samani katika eneo la Yambio, jimboni Equatoria Magharibi.

Malis ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 26, alitekwa nyara na kundi la watu wenye silaha akiwa barabarani na akapelekwa msituni, ambako aligeuzwa askari wa msituni.

Mwenyewe ana simulizi:"Wakati tulipokuwa msituni, tulipata shida sana. Amani ilipopatikana nchini mwetu, tulitoka msituni na kujisalimisha na tulipatiwa mafunzo."

Mapema mwaka 2018, ndiyo ilikuwa mwanzo wa faraja na ukombozi wa Malis, akiwa na baadhi ya wenzake alisema, ndipo alipobahatika kuachiwa huru, ikiwa ni zao la kazi ya utetezi na upatanishi zilizoongozwa na vikundi vya kidini na ujumbe wa Umoja wa Mataifa, nchini Sudan Kusini UNMISS.

Askofu Hiiboro Kusala, wa Kanisa Katoliki Dayosisi ya Tombura na Yambio, ni Mwenyekiti wa kikundi cha wapatanishi wa kidini na anazungumzia harakati za kuachiliwa Malis na wenzake akiufafanuya kwa kauli:

"Tuliweza kukutana na watu hao msituni na kisha kuwatoa msituni zaidi ya vijana 10,000 waliokuwa wanashikiliwa huko, vijana ambao walikuwa tayari kuua na hata kupigana.

"Ni kwamba mara nyingi, jambo ambalo sipendi kusema, vijana hao walikuwa wanatufanyia manyanyaso sana msituni, lakini hatukukata tamaa," anaeleza Askofu.

Kunasuliwa msituni kwa vijana hao, kumewezesha leo hii Malis awe na stadi za ufundi seremala, akiwa na cheti baada ya kumaliza mafunzo ya miezi sita ya ufundi stadi, yaliyofadhiliwa na UNMISS na wadau, na ikatekelezwa na shirika la World Vision katika chuo cha mafunzo stadi cha Tiindoka.

Malis anachangia mada: "Nilianza kujifunza jinsi wanavyopima vitu vyote, mfano kukata na kuweka matundu. Nilijifunza vitu vyote hapo sasa naweza kutengeneza meza, viti na hata vitanda. Mtu anaweza kufika akapenda na tunazungumza na ananipatia fedha."

Ni mafunzo yaliyomuweza kuanzisha karakana yake na kutengeneza samani zinazohitajika kwenye jamii yake, akiwa sasa na wasifu mwingine, kwamba daima si mchoyo wa ujuzi wake.

Hivyo katika karakana yake, anafundisha vijana wengine, miongoni mwao ni Isaac (naye si jina lake halisi), anayesema: "Amenifundisha mambo mengi. Hivi sasa naweza kutengeneza vitu vingi kama vile vitanda, milango, kabati na vitu vingine vingi vidogo vidogo."

UNMISS kwa upande inajivunia mafanikio hayo kwa kuwa kwa kufanya kazi na wananchi wa Sudan Kusini katika kujenga amani ya kudumu ndio jukumu lake.

Christopher Muchiri Murenga, ni mkuu wa ofisi ya UNMISS mjini Yambio na anasema kuwa: "Tunataka kujenga mashauriano kati ya jamii kuhusu kile walicho nacho na fursa za maendeleo kwenye jamii zao na changamoto wanazokabiliana nazo.

"Vitisho wanavyodhani wanaweza kukumbana navyo na uthabiti na udhaifu wao, ili hatimaye wao wenyewe wawe vichocheo vya kujenga upendo na kusonga mbele katika kujikwamua na kuendelea."

Kwa mujibu wa shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (Unicef), zaidi ya watoto 3,000 nchini Sudan Kusini wameachiliwa huru na vikundi vilivyojihami tangu kuanza kwa mapigano ya wenyewe nchini Sudan Kusini, mwezi Desemba, mwaka 2013 na kuna idadi kubwa wanaotumikishwa vitani.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za UN.***



Kijana Malis, akiwajibika ndani ya karakana yake ya useremala. **PICHA: UN**

> **"Ni kwamba mara nyingi, jambo ambalo sipendi kusema, vijana hao walikuwa wanatufanyia manyanyaso sana msituni...**

UCHUMI

KAZI YA TARI

# Serikali inayopambana kuweka juu mafuta ya michikichi ivuke Kigoma

## • Inaratibiwa na watafiti, nyenzo mbegu mpya

**Na Frank Kaundula**

KATIKA uhalisia uliopo hivi sasa nchini, Tanzania haijitoshelezi katika uzalishaji mafuta ya kula ya kila siku, hata kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi. Maana halisi ni kwamba zinatumika hata fedha za kigeni kuagiza ili kuziba pengo la mahitaji ya kitaifa.

Uhalisia unaeleza michikichi ndio zao linalotajwa kutoa mafuta mengi zaidi kulinganisha na mengine kama vile alizeti, pamba,ufuta na karanga. Hicho kimeifanya serikali kuipa kipaumbele zao hilo.

Ni katika muktadha huo,Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amekuwa mfuatiliaji kuhakikisha nchi ama inajitosheleza au kupunguza kiwango kikubwa cha uagizaji mafuta ya kula na zao la kimkakati chikichi, linalolimwa kwa wingi Kigoma.

Akiwa mkoani Kigoma, Waziri Majaliwa aliagiza mamlaka ya mkoa na halmashauri zake kuhakikisha wanasimamia kwa umakini usambazaji wa mbegu bora za zao hilo, ili kuongeza tija kitaifa.

Mbegu bora aina ya Tenera inazozalishwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) na Waziri Mkuu alipokuwa katika kituoa cha Kihinga kukagua maendeleo ya uzalishaji mbegu bora za michkichi, aliwaeleza:

"Tunataka nchi yetu ijitosheleze kwa mafuta ya kula na chikichi ndiyo linalitoa mafuta kwa wingi, hivyo nawaagiza wakuu wa wilaya zote, wakurugenzi na maofisa kilimo, kuhakikisha zao hili linalimwa sana hapa Kigoma," anatamka Majaliwa.

Ni agizo linalowajumuisha viongozi hao, pia maofisa kilimo kufuatilia mbegu bora aina ya Tenera na kuzifikisha kwa wakulima, akiwahakikishia itawapa tija ya kipato cha kutosha na wakati huohuo, nchi itajitosheleza kwa mafuta.

Salamu ya maofisa kilimo ilikuwa ni kuhakikisha wanashirikiana kwa karibu na walima chikichi, kwa kukifanya kilimo chao kiwe chenye tija, hali inayoifikia taifa zima kukwea kiuchumi.

Pia, Majaliwa anatumia fursa hiyo kuwapongeza watafiti wa Tari kupitia Mkurugenzi Mkuu, Dk. Geoffey Nkamilo, kwa kufanya utafiti wenye mafanikio makubwa yenye sura ya kuchangia mafanikio.

"Nimefurahishwa sana kwa jinsi mlivyofanya utafiti, kuzalisha na kusambaza mbegu bora za michikichi 1,525,017 aina ya Tenera. Naomba muendelee na moyo huo kwani sisi kama nchi tunajivunia uwepo wenu nyinyi," anasema Majaliwa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiangalia kitalu cha miche ya michikichi aina ya Tenera, alipotembelea Kituo cha Utafiti wa Kilimo (Tari), Kihinga, mkoani Kigoma.

> **"Nimefurahishwa sana kwa jinsi mlivyofanya utafiti, kuzalisha na kusambaza mbegu bora za michikichi 1,525,017 aina ya Tenera.**

### MKURUGENZI TARI

Mkurugenzi Mkuu wa Tari Dk Geoffrey Mkamilo, awali kuhusu utafiti, uzalishaji na alianisha hatua kadhaa za kushughulikia.

Dk Mkamilo anaeleza kwa hatua kwamba, wakati uoteshaji huchukua miezi mitatu, kitalu cha awali nacho kinachukua muda kama huo, kisha inahamishiwa kitalu kikubwa kwa miezi sita.

Anarejea kazi iliyokwishafanyika hadi Februari 15 mwaka huu, walishazalisha jumla ya mbegu 1,525,017 zilizopandwa katika shamba la ekari 30,500

Bosi huyo wa Tari anasema asilimia 33 ya kilichozalishwa ni kutoka sekta binafsi, hatua iliyowezesha wakulima wengi nchini kujiunga katika kilimo hicho.

Kwa mujibu wa Dk. Mkamilo, Tanzania inatumia takribani tani 570,000 za mafuta ya kula kila mwaka na tani 365,000 (wastani asilimia 60) ya mafuta yanayotumiwa nchini yanaagizwa kutoka nje ya nchi.

"Hali hii haitakiwi kuwapo kwani Tanzania ina ardhi ya kutosha na hali ya hewa inayofaa kwa uzalishaji wa mafuta ya kula, hivyo wanakulima wanatakiwa kutumia fursa hii kulima zao la chikichi kwa wingi hapa nchini," anasema Mkamilo.

Anasema ni sababu ya Tari kuweka juhudi za ziada kuwa na maboresho na hata kuzindua vituo vipya vya kuzalisha na kusambaza mbegu bora katika kanda zake; Magharibi, Kati na Kusini.

Pia, katika Nyanda za Juu Kusini na Kusini, mkurugenzi huyo wa Tari, anasema tayari mbegu bora zaidi ya milioni moja na nusu zimeshasambazwa kwa wakulima walioonyesha hamasa ya kuwekeza kwenye kilimo cha chikichi.



Mbegu ya mchikichi na mafuta yake yaliyokwishakamuliwa. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

### CHANGAMOTO

Dk. Mkamilo anasema, bado kuna upungufu wa mbegu bora, hali anayoamini itapatiwa ufumbuzi, kutokana na hamasa ya juhudi za wakulima.

Pia, anataka changamoto ya wakulima kuendelea kutumia mbegu kongwe za michikichi na utoaji wake wa mafuta ni mdogo sana kulinganisha na mbegu mpya, ambazo ni bora kwa kilimo hicho.

Dk. Mkamilo anataja ukosefu wa elimu na uelewa mpana kuhusu faida na manufaa yatokanayo na kinachowasukuma baadhi ya wananchi washindwe kwenye maeneo ya mikoa yao.

Benjamin Onesmo, ni mkulima wa mahali hapo, anayeomba usambazaji mbegu uwalenge hasa wakulima wanaoishi maeneo mengi ya vijijini.

Onesmo anasema wakulima vijijini wengi wamehamasika, lakini wanakabiliwa na changamoto ya kutopata mbegu kwa wakati, kitendo kinachowakatisha tamaa. Anaiomba Tari iliangalie suala hilo kwa makini

### MIKAKATI IKOJE?

Dk Mkamilo anasema Tari kitaifa imejipanga kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha kilimo bora cha michikichi nchi nzima na tayari wametoa mafunzo kwa halmashauri mbalimbali, ili kuhakikisha dhamira hiyo inafanikiwa.

Anasema Tari tayari imeshatoa mafunzo kwa halmashauri, wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Kilimo (Mati) Mubondo, watafiti na maofisa ugani, pia wawezekaji kuhusu manufaa ya kilimo cha michikichi, hata kupitia vyombo vya habari.

Taasisi ya Tari ipo chini ya Wizara ya Kilimo, ikiwajibika kisheria kwa majukumu ya kutafiti, kusimamia, kuhamasisha na kuratibu utafiti wa kilimo nchini.

Katika kutimiza majukumu yake, Tari ina kurugenzi tatu ambazo ni za: Utafiti na Ubunifu, Biashara na Uhusiano na Utawala na Rasilimali Watu, ikiwa na jumla ya wafanyakazi wastani 700, kati yao asilimia 75 ni watafiti.

Dk. Mkamilo anagusia walivyojipanga kwa mikakati yao kuzalisha mbegu bora za kusambaza kwa wakulima katika maeneo yote yanayofaa kwa michikichi, akiwapa hamasa walioko nje ya Kigoma wazalishe michikichi.

Anasema, pia Wizara ya Kilimo, imetengea bajeti Sh. bilioni 2.9 za kuboresha miundombinu ya kituo cha Kihinga, inayojumuisha maeneo ya ofisi, maabara na usimamizi wa mbegu, ili kuweza kuongeza tija kwa maslahi kitaifa.

Kwa mujibu wa Dk, Mkamilo, Kituo cha Tari Kihinga kilichopo Kigoma kilianzishwa Julai, mwaka 2018 na kupewa ardhi ya ekari 540.24 kwa ajili ya uendelezaji mchikichi mkoani humo na maeneo jirani nchini.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hodi hodi wananzengo!






**NA JOSEPH KULANGWA**

WASALAAM Aleykoum ndugu wasomaji na wananzengo wote. Baada ya mimi kukaribishwa kutoa nilichonacho ndani ya ubongo wangu na kukianika hapa, nami kwa mikono mikunjufu kabisa nakukaribisheni katika safu hii itakayojulikana kama Tafakuri ya Mlalahoi.

Safu hii kama inavyojibainisha, itakuwa imebeba mawazo yangu mlalahoi, pengine kwa niaba ya walalahoi wenzangu katika Taifa hili, kwa lengo na dhima nzima ya kuchambua maisha ya kila siku kijamii, kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na burudani.

Mimi si mgeni saana katika medani hii, kwani huko nilikokuwa kabla ya kuhamia hapa, nilijaribu kuwa nafanya hivi, nikitumia taaluma inayowezesha kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha. Lakini mara nyingi mimi huongeza pia kukosoa, kupongeza, kusifia inapobidi na kutia moyo ili maisha yasonge mbele.

Safu hii haitajiabudisha katika itikadi ya chama chochote cha siasa, ingawa mara nyingine itapambana na itikadi yoyote itakayotaka kuwatoa wananchi kwenye reli, hususan walalahoi ambao wanahitaji usaidizi wa kifikra.

Naamini wasomaji wangu mtanipokea na tutakuwa sambamba katika kuelimishana, kuhabarishana na hasa kukosoana pale tutakapokuwa tunapotoka, kwa lengo jema la kuisaidia nchi yetu katika kuendeleza mapambano ya kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Tunapitia kipindi kigumu hivi sasa cha kiuchumi, huku pia pembeni tukikabiliwa na janga la gonjwa la corona ambalo hatuna budi kukabiliana nalo pamoja na upya wake. Naamini kwa kushirikiana, litatokomea na kutuacha kama tulivyokuwa huko nyuma.

Pamoja na hali hiyo, bila shaka wakati mwingine usemi wa baniani mbaya kiatu chake dawa, unajidhihirisha katika mapambano haya. Kabla ya ziara ya corona a.k.a Covid-19 duniani hasa huku kwetu, tabia ya kunawa mara kwa mara ilikuwa haba, tuseme ukweli tu. Leo watu wananawa sana tu.

Swahiba mmoja jirani yangu amediriki kuniambia kuwa ndiyo maana hatusikii milipuko ya kipindupindu, kwa sababu tunanawa. Kumbe huko nyuma tulikula bila kunawa, hivyo kukaribisha kina Salmonela waliotufanya tuharishe na kutapika ovyo na hata kupoteza maisha.

Tuliambukizana kifua kikuu tulipobanana kwenye vyombo vya usafiri, leo hii tunakaa kwa kujinafasi, kuchelea kuambukizana corona. Tulipumuliana hewa chafu na kutemeana makohozi na kupengeana makamasi tulipopiga chafya na kukohoa, leo hii barakoa ziko kazini.

Hebu fikiria wakati ule tukisafiri kwa mabasi kwenda mikoani, mnafika mahali ghafla unamwona mmoja wa abiria anatoka nyuma ya basi anakimbilia kwa dereva anamnong'oneza kitu, mara unaona basi linaegeshwa pembeni na kutoka tangazo:

Anakufuata anakukumbatia, anakupetipeti na mnashikana mikono. Unajua kabisa katoka ama haja kubwa au ndogo kichakani, unajua kabisa huko alikotoka hakuna bomba la maji tiririka, kuna majani na matawi ya miti. Anakushika mikono, mnashikana na kucheka.

Mnapanda basi, anaomba ahamie ulipokaa na kubadilishana na abiria mwingine ambaye hamkuwa mnapiga michapo. Alipokaa hapo mlipo pamoja na michapo, haachi kujikuna makalioni, kwa sababu alichokifanya porini kakosea majani katumia ya jamii ya upupu.

Mara basi linasimama kituo fulani wanakuja wa mahindi ya kuchoma, ananunua na kukukatia, mnajichana. Ghafla unasikia mngurumo kama wa treni tumboni. Hapo kazi inaanza, kama si kuhara, omba Mungu. Leo hii na corona hii nani akubali hayo? Ni mwendo wa majitiririka na sanitaiza.

Corona anatutesa na kutupokonya maisha yetu na ya wapendwa wetu, lakini anatuachia pia somo la usafi na kujijali. Akiondoka tutakuwa nasi tumejua nini cha kufanya na nini cha kuacha, huku pia bila shaka akiwa ametuachia pia waganga wengi wa jadi. Alamsiki.

BIASHARA

# Ubia wa REA inaposhikamana na Wakala Misitu kuwasha umeme

- Umeme 'bwelele' vijijini, nguzo za nyumbani
- Wawekezaji nguzo kibao 'mteja wa uhakika'



Nguzo za umeme zikisombwa vijijini, tayari kupelekewa mteja wake, REA.

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

NI miaka mitano sasa, kuna hatua kubwa imepigwa katika usambazaji umeme nchini, hasa katika dhana kuu ya kuufikisha katika vijiji vingi kitaifa.

Mdau mkuu hapo ni Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kazi hiyo ikifanyika kwa taratibu na gharama nafuu zaidi chini ya malezi makuu ya kisera kutoka serikalini, mlezi na msimamizi mkuu Wizara ya Nishati.

Ni mradi unaofanyika kwa awamu kuzunguka maeneo mbalimbali ya vijijini, mtazamo mkuu ni kumaliza kila kona ya vijijini kitaifa.

Ni kazi ya kiufundi inayofanywa na REA, ikihusisha matumizi ya rasilimali nyingi kama fedha, nguvu kazi na vifaa vya umeme kama nyaya za na nguzo za kusafirisha umeme.

**KAZI YA TFS**

Ili kufanikisha, kunaibuka hitaji la vifaa hivyo vipatikane kwa wakati na gharama nafuu. Hapo ndipo panatokea hitaji la sekta misitu, mhusika na mnufaika mkuu katika utoaji mchango chanya katika jitihada za serikali na usambazaji umeme.

Sekta misitu ina manufaa katika maeneo makuu mawili. Kwanza, upatikanaji malighafi ya nguzo zenye ubora na kubwa tofauti; pili kuruhusu umeme kupita katika maeneo ya misitu bila ya fidia.

Misitu ya serikali inayozalisha nguzo imenufaika sana na biashara ya miti ya kutengenezea nguzo,

> **"Bila misitu, hatuwezi kupata miti ambayo itatengenezwa nguzo za umeme, hatuwezi kupata mbao ambazo hutumika kutengeneza fenicha mbalimbali ambazo huitajika katika matumizi ya binadamu.**



Wanufaika wa umeme wa REA kwa 'raha zao' kijijini wakifaidika na kazi ya nguzo. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

hali kadhalika mashamba ya wananchi na asasi nyingine binafsi.

Mashamba ya miti ya serikali yanayosimamiwa na kuendelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), yamekuwa mstari wa mbele katika ufanisi wa kutoa miti bora ya kutengenezea nguzo za umeme.

Baada ya kuliona hilo, TFS nayo imekuwa ikijitahidi kupanda miti mipya kila baada ya mavuno, kuhakikisha nguzo zinazohitajiwa na REA zinapatikana wakati wote kwa namna endelevu.

Kamishna wa TFS, Dos Santos Silayo, anasema wanahudumia wateja 186, wakiwamo Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco), inayovunwa kutoka mashamba yake nchini.

Anasema wateja hao huvuna wastani wa nguzo zenye ukubwa wa mita za ujazo 150,000 kwa mwaka, ikiwa biashara iliyoibua fursa kubwa katika uwekezaji wa misitu nchini, ikihususha wadau mbalimbali.

Silayo anatumia fursa hiyo kusifu uamuzi wa serikali kuuwekeza kwenye teknolojia ya kutibu nguzo na anarejea takwimu za ndani ya kuwapo uwezo wa viwanda kuruhusu umeme kupita katika misitu bila ya fidia.

Hadi sasa inaleezwa ni hatua kubwa inayopigwa ikizingatiwa nguzo hizo zinazozalishwa nchini, awali ziliagizwa kutoa nje ya nchi.

Miti hutumia hewa chafu ya ukaa kutengeneza chakula chake na kisha miti hiyo inapotumika kama malighafi huhifadhi kaboni kwa muda mrefu bila kuiachia angani.

TFS, inawapongeza waliowekeza katika malighafi nguzo, akizitaja kampuni za misitu zilizowekeza katika uzalishaji wake nchini, hali inayoiwezesha nchi kuwapiku washindani wakongwe, viwanda vya Kusini mwa Jangwa la Sahara ambako bidhaa hizo zilozgizwa awali.

Uamuzi wa kutumia nguzo za ndani ulitolewa na serikali na kuachana na dai la kwamba 'nguzo za nchini hazina ubora' na matinda yake ya sasa, ni kwamba biashara hiyo imeongezeka maradufu na nyenzo ya kukabili tabia nchi.

Silayo anakumbusha wajibu wa umma, kila mmoja anapaswa kuzingatia wajibu wa kutunza misitu iliyopo, ili isaidie kutoa nguzo za umeme zinzotumiwa kwa ajili ya kuwawekea watu umeme katika maeneo ya mijini na vijijini.

Kamishna Silayo anasistiza wito wa TFS, kwamba kila mwananchi ahakikishe anakuwa mlinzi wa mwenzake, katika kuhakikisha ibaki salama.

**WADAU MISITU**

Mmoja wa wananchi wanaoishi jirani na misitu, Jerome Massawe, anaunga mkono hoja hiyo, akihimiza kwamba misitu inapaswa kuheshimiwa na kutunzwa, kwa sababu ni mzizi wa faida kubwa kwa wananchi na taifa kwa jumla.

"Bila misitu, hatuwezi kupata miti ambayo itatengenezwa nguzo za umeme, hatuwezi kupata mbao ambazo hutumika kutengeneza fenicha mbalimbali ambazo huitajika katika matumizi ya binadamu," anasema.

Asia Juma, mdau mwingime wa rasilimali misitu anasema wananchi wana kila sababu ya kutunza misitu inayowazunguka, kwa sababu ina faida kubwa kuanzia ndani ya jamii yao, hata taifa kwa jumla.

Mama huyo anaorodhesha faida hizo mtambuka, zinazojumuisha uchumi na mazingira, anazitaja kuwa inaleta mvua, hali ya hewa nzuri na matumizi na malighafi kwa mengi ya miradi ya kiuchumi na kibiashara.

Kutokana na mustakabali huo, Asia anahimiza jamii kuzingatia utunzaji na kuheshimu misitu kila wakati na njia mojawapo anayoshauri ni kwamba kila anyemuona mkata misitu ovyo jirani, anapaswa kuchukua hatua ya kumripoti haraka katika mamlaka husika za kiserikali zinazosimamia hifadhi zake, ili hatua sahihi ichukuliwe.



HABARI DODOMA

# Chikota ataja siri h/shauri kupata hati inayoridhisha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amesema uwepo wa nidhamu ya matumizi ya fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa umechangia asilimia 95 ya halmashauri kupata hati inayoridhisha kwenye ukaguzi.

Chikota ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), alitoa kauli hiyo bungeni alipokuwa akichangia hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2019.

Alisema taarifa ya CAG inaonyesha kuwa kati ya halmashauri 185 zilizokaguliwa, halmashauri 176 imepata hati inayoridhisha sawa na asilimia 95 na imetokana na nidhamu hiyo pamoja na usimamizi mzuri uliopo.

Alieleza kuwa hatua hiyo ni maboresho makubwa ikilinganishwa na kipindi cha nyuma wakati halmashauri nyingi zilikuwa zinapata hati yenye mashaka, lakini kwa sasa ni halmashauri 9 sawa na asilimia 5 tu ndio zimepata hati yenye mashaka.

Hata hivyo, alisema pamoja na maboresho hayo bado kuna maeneo ya kufanyia kazi ikiwamo kwenye taratibu za manunuzi ambapo imeonyesha kuna ukiukwaji.

"Kwenye vitengo vya manunuzi ya serikali za mitaa kumeimarika kwa kiasi kikubwa lakini bado kuna dosari kama CAG alivyoonyesha kuwa amefanya ukaguzi wa kina katika halmashauri 74 na kukuta kuna manunuzi ya Sh. bilioni 32.4 yamefanywa bila ya kushindanisha kama sheria ya manunuzi inavyotaka," alisema.

Aliongeza: "CAG pia amefanya ufuatiliaji wa kina kwenye mamlaka za serikali 47 na kukuta manunuzi yamefanyika bila ya kutumia 'tender board' na hii imechukua kama Sh. bilioni 9.2, hapa ofisa masuhuli angeweza kuzuia hoja hizi kwa kutumia 'tender board' ambayo ipo kisheria kwenye mamlaka za serikali za mitaa."

Aliomba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kufuatilia udhaifu kama huo kwa halmashauri husika ambapo taarifa ya CAG ipo wazi na imezitaja halmashauri hizo.

"Tujiulize kwa nini maofisa masuhuli wameamua kufanya hivi maana wanaturudisha nyuma, hoja kama hizi hazikuwa na sababu ya kuwapo kwenye taarifa kama hii," alisisitiza.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalanganya, akikabidhi cheti kwa mwenye ulemavu, Bashiru Kajuna, baada ya kuhitimu mafunzo ya udereva wa bajaji, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

## Wenye ulemavu watakiwa vikundi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU wenye ulemavu nchini wametakiwa kuunda vikundi vya uzalishaji mali na kuvisajili kisheria serikalini, ili wavitumie kupata mikopo ya asilimia mbili, inayotolewa na halmashauri.

Rai hiyo ilitolewa jana na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalanganya, alipokuwa akizungumza na walemavu wahitimu wa mafunzo ya udereva wa bajaji.

Alisema wanatakiwa kuchangamkia fursa ya mikopo ya asilimia mbili inayotolewa maalum kwa ajili yao ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Nabalanganya alisema katika mwaka huu wa fedha tayari wameshatoa mikopo ya asilimia mbili kwa vikundi 12, vya watu wenye ulemavu kwa Jiji la Dodoma ambapo takribani Sh. milioni 120, zimetumika.

Aidha, alivitaka vikundi ambavyo vimekuwa vikipata fedha za mikopo ya halmashauri kuzitumia vizuri katika maeneo yaliyokusudiwa na siyo vinginevyo.

Alisema kumekuwapo na tabia kwa vikundi hivyo kukopa fedha na kugawana badala ya kutumia katika vifaa vilivyopangwa kulingana na mkopo unavyoelekeza.

"Sasa hivi wapo maofisa wangu ambao wanafuatilia na kuhakikisha kuwa vikundi vyote vinavyopata mikopo wananunua vitendea kazi na siyo kugawana fedha, watu wengi wanakimbia mikopo kutokana na kushindwa kurejesha kutokana na kugawa fedha na kuzitumia kinyume," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wahitimu wenzake wa mafunzo ya bajaji, Wema Hassani alisema kuwa mafunzo hayo yatawawezesha kupatiwa mkopo wa bajaji waliomba katika kampuni ya Ashton Foundation ya Jiji Dar es Saalam.

Alisema kuwa ni matumaini yao kuwa mkopo wa bajaji utawawezesha walemavu wa mkoa wa Dodoma kujikimu kimaisha na kutoacha kuwa tegemezi.

Mwenyekiti wa Taasisi inayojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu wa aina zote (Tasodefa), Paul Mahanyika, aliwataka walemavu kuacha kuwa wanyonge bali wapambane katika kujikwamua kiuchumi.

# Agizo waratibu wazembe wa Tarura watumbuliwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameuagiza Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) kuwaondoa waratibu wa mikoa wazembe ambao wanakwamisha utendaji kazi wa wakala huo.

Pia, ameagiza kuvunjwa kwa kamati za manunuzi ambazo zinasababisha kuchelewa utekelezaji wa miradi ya barabara kwenye maeneo yao licha ya serikali kutoa fedha.

Jafo alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akizindua Bodi ya kwanza ya Ushauri ya Tarura ambayo mwenyekiti wake ni Florian Kabaka.

Alisema kuna baadhi ya maeneo kuna waratibu hao kazi hazifanyiki na kuwataka vongozi wa wakala huo kuwa wakali na kuondoa watendaji wote wazembe.

"Kuna waratibu wa mikoa magoigoi waondolewe na kamati za manunuzi ambazo hazifanyi kazi wakati fedha zipo zivunjwe," alisema.

Aliongeza: "Pitieni na mfanye mabadiliko ya kamati hizo, kuna fedha zilitolewa na Rais Sh. bilioni 33 kuna maeneo bado yanaendelea na mchakato wa manunuzi wakati wengine wapo mbali kwenye utekelezaji."

Jafo alisema Tarura kwa kiwango kikubwa inategemea fedha kutoka Mfuko wa Barabara ambapo inapata asilimia 30, huku Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) ikipata asilimia 70.

"Kuna kazi kubwa inafanyika ya kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine ikiwamo DFID, Benki ya Dunia, uwepo wenu bodi utasaidia kubuni mambo mengine ya kusaidia Tarura iweze kuhudumia wananchi," alisema.

Alisema Tarura ina mtandao wa barabara 108,950 fedha zilizopo ni ndogo, na kuitaka Bodi kuhakikisha rasilimali fedha zilizopo zinatumika kwa nidhamu.

"Viongozi na watumishi wa umma tujenge tabia inayolenga kuwasaidia wananchi tusijenge tabia ya ubinafsi na umimi, tumesema mvua zimenyesha mtandao wa barabara umeharibika zaidi, asilimia 23 ya barabara ndio zipo wenye hali nzuri," alisema.

Aliitaka bodi kujipanga kuhakikisha Tarura inafanya kazi vizuri kwenye utengenezaji wa barabara hizo kwa kutoa ushauri wa nini kifanyike ili fedha zipatikane za kukarabati barabara.

"Kama sisi tutasema tumeacha ubinafsi tunaweza kwenda mbali zaidi hata kama rasilimali ni chache, nendeni mkafanye kazi ya kutafuta fedha, katafakari kwa kina nini kifanyike kwa kipaumbele," alisema.

Jafo alisema tangu kuanzishwa kwa Tarura, taasisi hiyo imefanya kazi kubwa ya kuhudumia mtandao wa barabara jambo ambalo limeifanya kujijengea heshima na wadau wakiwamo wabunge wakitetea suala la ufinyu wa bajeti.

"Hali ya barabara upande wa miji ilikuwa mbaya, mradi zaidi ya Sh. bilioni 820 ndio inabadilisha miji yetu, ukiona barabara nzuri, taa ni kazi kubwa imefanywa na Tarura," alisema.

# Shivyawata masharti mikopo kuangaliwa upya

**Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (Shivyawata), Mkoa wa Mbeya limeiomba serikali kuangalia upya masharti ya utoaji mkopo wa asilimia mbili kutoka halmashauri ili kundi hilo linufaike na kumudu gharama za maisha hasa katika kipindi hiki cha janga la ugonjwa wa Covid-19.

Ombi hilo lilitolewa jana na shirikisho hilo wakati wakipokea msaada wa ndoo tano za kunawia mikono ili kukabiliana na janga la ugonjwa wa Covid-19 ambazo zilitolewa na Naibu Waziri wa Kazi, Vijana anayeshughulika na watu wenye ulemavu, Stella Ikupa.

Akizungumzia suala la mikopo kwa watu wenye ulemavu, Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona (TLB), mkoani humo, Joseph Mwandalima, alisema kipindi hiki cha janga la corona hali ya kiuchumi imekuwa mbaya kwao.

Alisema hata mikopo inayotolewa na halmashauri imewekewa masharti magumu hali inayosababisha kukosa sifa ya kukopesheka na kuiomba serikali kuangalia upya ni kwa namna gani watalisaidia kundi la wenye ulemavu kupata mikopo.

"Miongoni mwa masharti ambayo halmashauri zetu imeweka kwenye mikopo yao ni kwamba kila kikundi lazima wapate usajili na barua kutoka kwa watendaji wa vijiji, sisi wenye ulemavu tumetawanyika unashangaa wawili wako kijiji kimoja na wengine wako mbali sasa ni ngumu kuunganika kwa pamoja cha muhimu watuhimize tujisajili bila kujali tunatoka kijiji kimoja," alisema Mwandalima.

Aliongeza kuwa hali ya sasa kiuchumi kwao ni mbaya kuliko ugonjwa wenyewe wa corona, lakini aliwahamasisha wenzake kuendelea kuchapa kazi kwa kufanya shughuli ndogo ndogo za kujiingizia kipato.

Mwenyekiti wa Shivyawata Mkoa, Luca Mahenge, alisema licha ya kuwapo kwa idadi ndogo ya waliopo au kufariki kutokana na janga la corona, haiondoi uhalali kwamba wako kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa kutokana na tatizo la ukosefu wa vifaa vya kujikinga.

Alisema msaada wa Naibu Waziri Ikupa ndio wa kwanza kuupata tangu janga hilo liripotiwe nchini, wadau na serikali imewasahau katika vita hivyo licha ya kuwa uhitaji bado ni mkubwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu (Chawata) mkoa, Jimmy Ambilikile, alisema msaada wa ndoo kwa ajili ya kunawa mikono utagawiwa katika kila ofisi ya chama cha watu wenye ulemavu na wanahitaji dawa na sabuni za kunawia.

Aliwaomba wadau na serikali kuendelea kuwasaidia vifaa mbalimbali vya kujikinga kwa kuwa ndoo hizo hazikidhi mahitaji kutokana na kila wilaya kuhitaji vifaa hivyo.



Mwenyekiti wa Chama cha Watu wasioona Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwakitalima (kushoto), akipokea msaada wa ndoo ya kunawia mikono ili kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu mkoani humo, Jimmy Ambilikile, kwa niaba ya Naibu Waziri wa Vijana, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Stella Ikupa, katika hafla iliyofanyika jijini humo jana. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu Shivyawata, Luca Mahenge. **PICHA: GRACE MWAKALINGA** .

# Mahakama yazuia dhamana ya Mdude

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Mbeya, imezuia dhamana ya mfuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mdude Nyagali, kufuatia maombi yake yaliyotolewa na upande wa utetezi katika kesi ya jinai inayomkabili.

Sababu za kuzuia dhamana hiyo ni kutokana na mabadiliko ya kifungu cha sheria namba 13 ya kudhibiti dawa za kulevya ya mwaka 2017 na mtuhumiwa alirejeshwa rumande hadi Juni 3, mwaka huu huku akifunguliwa kesi nyingine ya jinai namba 136 ya mwaka 2020.

Mei 13, mwaka huu, Mdude alifikishwa katika mahakama hiyo akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine zenye uzito wa gramu 23.4.

Mahakama hiyo ilimfutia shtaka la awali la uhujumu uchumi kulingana na kifungu cha 91 (1) cha sheria ya mwenendo wa mashauri ya jinai.

Mwendesha mashtaka wa Serikali Mwandamizi, Basilius Namkambe, akishirikiana na Lugano Mwakilasa, waliieleza mahakama kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) alionyesha nia ya kutotaka kuendelea na shauri hilo maombi yaliyopokelewa na mahakama.

Baada ya kufutiwa kosa la awali, upande wa Jamhuri uliiomba mahakama kwa mara nyingine kumfungulia mtuhumiwa shtaka la jinai la kusafirisha dawa za kulevya kinyume na mabadiliko ya sheria ya kudhibiti dawa za kulevya kifungu namba 15A (i) kama ilivyorejewa mwaka 2017.

Mabadiliko hayo ya sheria yalifuta kifungu cha 29 cha sheria ya dawa za kulevya kilichokuwa kikiruhusu mtuhumiwa kupewa dhamana kwenye dawa za kulevya zinazozidi gramu 20.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Reginald Martine na Faraji Mangula, uliomba mahakama hiyo kumpatia dhamana mteja wao kama ilivyo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 13 wakirejea maamuzi ya Mahakama Kuu katika kesi ya Dickson Sanga, dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliyotolewa uamuzi Mei 18, mwaka huu kwenye jopo la majaji watatu likiongozwa na Jaji Masoud.

Katika uamuzi huo, Mahakama Kuu ilisema makosa yote yasiyokuwa na dhamana ikiwamo unyang'anyi wa kutumia silaha chini ya kifungu cha 148 cha mwenendo wa makosa ya jinai sura namba 20 kama ilivyorejewa mwaka 2019 yapewe dhamana.

Mahakama ilieleza kufahamu uamuzi huo wa Mahakama Kuu, lakini ikabainisha kwamba haiwezi kuufuta kwa sababu serikali imepewa miezi 18 kuirekebisha sheria inayozuia dhamana na kwamba bado pia miezi 18 haijakamilika.

Licha ya uamuzi huo wa mahakama upande wa utetezi ulidai kukata rufani ya mdomo na maandishi Mahakama Kuu ili kutaka mteja wao apatiwe dhamana.

# Wakulima Mbarali kusajiliwa kuondolewa usumbufu

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, imetakiwa kuwasajili na kuwatambua wakulima wote hasa wa mpunga ili kuwaondolea usumbufu wa kukamatwa wanaposafirisha mazao yao kutoka shambani wakidhaniwa kuwa ni wafanyabiashara wanaokwepa ushuru wa mazao.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu wa Jukwaa la Wakulima na Wafugaji, Christopher Uhagile, wakati akizungumza na Nipashe na kusema kuwa sheria ndogo ya ushuru wa mazao inakiukwa kwa kuwalazimisha wakulima wanaosafirisha mazao yao kutoka mashambani kulipa ushuru kwa vile sheria hiyo inaelekeza anayepaswa kulipa ushuru huo ni mnunuzi wa mazao na sio mkulima.

Alisema ili kuondoa adha wanayokabiliwa nayo wakulima wanapotoa mazao yao shambani na kupeleka nyumbani, jukwaa hawana ubishi kwamba lazima ushuru ulipwe, lakini tatizo ni nani anatakiwa kulipa ushuru huo.

"Katika kutatua shida ya wakulima wa mpunga kutozwa faini, jukwaa nimeomba serikali ya wilaya kupitia watendaji wa vijiji kuwatambua wakulima wote ili iwe rahisi kuwatoza wafanyabiashara wanaostahili," alisema Uhangile.

Aliongeza kuwa serikali haina budi kuwatambua wanunuzi wa mazao vijijini na kupiga marufuku ununuzi wa mazao yaliyo mashambani kwa madai kuwa kitendo hicho kinaikosesha serikali mapato kutokana na wanunuzi wa mazao yaliyo mashambani kujifanya ni wakulima.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wakulima na Wafugaji, Matagili Mbigili, aliwataka wakulima wilayani Mbarali kuheshimu maeneo ambayo ni mapito ya mifugo ili kuepusha migogoro na ugomvi baina yao na wafugaji.

Alisema hata hivyo, serikali iliruhusu usafirishaji wa mazao yasiyozidi tani moja bila kulipiwa ushuru, fursa ambayo sasa imeanza kutumiwa vibaya na wafanyabiashara kukwepa kulipa ushuru wa mazao, lakini msamaha huo unawakandamiza wakulima wanaopata mavuno mengi yanayozidi tani moja, wanapoyasafirisha kutoka mashambani.

**serikali haina budi kuwatambua wanunuzi wa mazao vijijini na kupiga marufuku ununuzi wa mazao yaliyo mashambani**



# Wizara Kilimo yaridhisha wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi imeipongeza Wizara ya Kilimo kwa hatua kubwa za kazi za maendeleo ilizozifanya katika kipindi kilichopita.

Baadhi ni ununuzi wa mtambo wa chakula cha kuku, jambo ambalo litawaondolea usumbufu wafugaji na kujiamini katika shughuli zao za ufugaji.

Hayo yalielezwa na Mjumbe wa Nadir, Abdullatif Yussuf, wakati akiwasilisha ripoti ya kamati hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema pembejeo za kilimo zimepatikana kwa wakati mwaka huu, jambo ambalo limewapa faraja wakulima.

"Kamati inasisitiza ugawaji wa pembejeo hizo ufanyike kwa kuzingatia vigezo madhubuti ili kuzigawa kwa wakulima na kusababisha kuongezeka ufanisi wa kazi zao pamoja na kukuza pato la Taifa," alisema.

Alieleza kamati pia inaunga mkono na kuzipongeza juhudi za wakulima wa matunda na mboga nchini kwa kasi ya uzalishaji waliyonayo, hatua ambayo limesababisha upatikanaji wa matunda kwa karibu misimu yote ya mwaka na kuimarisha afya za wananchi.

Hata hivyo, alisema kamati ilishangazwa na kushuka kwa mapato ya kifungu kidogo ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani kutoka Sh. 104,160,000 mwaka 2019/2020 hadi Sh. 95,000,000 kwa mwaka 2020/2021 ikiwa ni nakisi ya jumla ya Sh. 9,160,000.

Nadid alisema nakisi hiyo ni kubwa tukizingatia kwamba taasisi yenyewe ni changa na inahitaji rasilimali nyingi ili iweze kusimama na kuendesha majukumu yake ipasavyo.

"Hata hivyo, tunaipongeza serikali kwa kuleta hapa barazani Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Utafiti wa Kilimo... umeshatiwa saini na mheshimiwa Rais wa Zanzibar, kwa kiasi kikubwa utaisaidia taasisi hii kukusanya mapato na kuandika maandiko tofauti kwa washirika wa maendeleo yatakayoitangaza na kuiongezea mapato taasisi hii," alisema.

Alieleza kamati ina matumaini makubwa na taasisi hiyo kwamba iwapo itajipanga vizuri, itaweza kufanya mageuzi makubwa katika maendeleo ya kilimo na misitu.

Akizungumzia Makadirio ya Mapato ya Uvuvi wa Bahari Kuu kifungu (1422067) yameongezeka kutoka Sh. 1,526,080,000 mwaka 2019/2020 hadi Sh. 2,500,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021, alisema kamati imeshangazwa na ongezeko hilo.

Hata hivyo, alisema kamati haikufurahishwa na taarifa kuwa baadhi ya maeneo na vikundi vilivyopatiwa vifaranga vya samaki wameshindwa kuvilea na kuvikuza, hivyo vimekufa bila ya kufahamika kama vilizalishwa chini ya kiwango au ni uchache wa maandalizi kwa wakulima waliokabidhiwa.

Alieleza kuwa ipo haja kwa wizara kujipanga vizuri kwa miradi kama hiyo nyeti na inayogharimu fedha nyingi ikiwamo kuwapatia elimu wananchi kabla ya kukabidhiwa vifaranga hivyo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akiushukuru uongozi na Bodi ya Benki ya Watu wa Zanzibar {PBZ}, kwa uamuzi wake wa kuchangia Sh. milioni 100 kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: OMPR– ZNZ**

# Zanzibar yajikita uchumi wa uvuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema Shirika la Uvuvi la Zanzibar (ZAFICO) kwa kutumia meli yake aina ya Sehewa 11 iliyonunuliwa kutoka Srilanka imeanza shughuli za uvuvi katika eneo la ukanda wa bahari kuu.

Eneo la ukanda wa bahari kuu linaelezwa kuwa lina utajiri mkubwa wa samaki.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mjawiri alisema uvuvi wa eneo la bahari kuu utaliwezesha shirika kuuza samaki ndani ya nchi katika soko la utalii pamoja na kusafirisha nje ya nchi.

Alisema shirika hilo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuhakikisha sekta ya uvuvi inaleta tija kwa taifa pamoja na kuwawezesha wananchi kuunda vikundi vya uvuvi.

Alieleza kuwapo kwa Shirika la Uvuvi kwa kiasi kikubwa kutaifanya sekta ya uvuvi kuongeza mchango wake kwa uchumi wa taifa.

"Mheshimiwa napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa juhudi zake katika kulifufua ZAFICO ili lifanye kazi za uvuvi katika mwambao wa bahari kuu na kupunguza tatizo la uhaba wa samaki," alisema.

Aidha, alisema ZAFICO inatarajiwa kununua boti nyingine tano kwa ajili ya shughuli za uvuvi kwa vikundi mbalimbali vya vijana waliopo katika maeneo ya ukanda wa bahari kuu na kwa ajili ya doria.

Mjawiri alisema Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imejipanga kuhakikisha uvuvi haramu unaotumia mitego iliyopigwa marufuku unadhibitiwa.

Alizitaja juhudi zilizochukuliwa katika kukabiliana na uvuvi haramu ni kufanya doria 172 katika maeneo yaliyotengwa ya hifadhi ya uvuvi wa mwambao Unguja na Pemba.

Alizitaja doria hizo ni ukanda wa hifadhi ya PECCA iliopo Pemba ambapo jumla ya doria 30 zilifanyika, huku ukanda wa hifadhi ya MIMCA iliopo Unguja jumla ya doria 41 zilifanyika.

Alieleza kuwa katika doria hizo jumla ya mitego ya samaki haramu 68 ilikamatwa na kuharibiwa ikiwamo nyavu zenye macho madogo ambazo hunasa samaki wa aina mbalimbali.

Alizipongeza kamati za uvuvi za halmashauri ya vijijini ambazo zimefanya kazi kubwa kupambana na uvuvi haramu, ikiwamo kusaidia kazi za doria.

# PBZ yasaidia mil. 100/- vita corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Bodi ya Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), imeiunga mkono serikali kwa kutoa mchango wa Sh. 100,000,000 katika kusaidia mapambano dhidi ya kukabiliana na virusi vya corona.

Mkurugenzi Mtendaji wa PBZ, Iddi Haji Makame, alieleza hayo wakati wa hafla fupi ya kukabidhi hundi ya fedha hizo kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, Mjini Zanzibar ambazo zimeshaingizwa kwenye akaunti ya mfuko wa corona.

Mkurugenzi huyo alisema uongozi wa Benki hiyo umezingatia kazi kubwa na ya kizalendo inayofanywa na madaktari na watendaji wa sekta ya afya, na kupendeekeza kuwa Sh. 40,000,000 za mchango huo wapatiwe wahudumu wa sekta ya afya.

Alisema Sh. 60,000,000 wamefikiria kuhudumia wananchi wa kaya zilizoathirika na virusi vya corona ambao waliwekwa katika kambi maalum muda ambao umekwamisha harakati zao za kimaisha za kujitafutia riziki za kila siku.

Akipokea mchango huo, Balozi Iddi, alisema inatia moyo kuona kwamba kasi ya kuenea kwa virusi vya corona imepungua sana katika visiwa vya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Alisema mchango wa PBZ umeonyesha watendaji hao kuguswa na janga hilo ambapo pia aliwashauri wananchi waendelee kushirikiana na viongozi, taasisi pamoja na wataalamu wa afya katika kuhakikisha corona ndani ya visiwa vya Zanzibar inabakia kuwa historia katika muda mchache ujao.

Aliwashukuru wananchi wa Zanzibar kwa ukubali wao wa kuitikia pamoja na kupokea maagizo yote yaliyokuwa yakitolewa na viongozi wao pamoja na ushauri wa wataalamu wa afya katika kuepuka vishawishi vinavyosababisha kuambukizwa na virusi hivyo.

Makamu wa Pili huyo aliuhakikishia uongozi na Bodi ya Benki hiyo kwamba mchango huo utatumika na kuelekezwa kwa walengwa.

**Uongozi wa Benki hiyo umezingatia kazi kubwa na ya kizalendo inayofanywa na madaktari na watendaji wa sekta ya afya, na kupendeekeza kuwa Sh. 40,000,000 za mchango huo wapatiwe wahudumu wa sekta ya afya.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALIYU KABEGA ABDUKARIMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.1688-0503 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BAHARI BEACH SEKONDARI mwaka 2016.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: DAR/MBU/RB/401666/2020.**

1157558

## Taarifa ya Kufungwa

**INATOLEWA TAARIFA KUWA** katika mkutano wa ziada wa **AKASA RESOURCES LIMITED** uliofanyika siku ya 31st ya December 2019, azimio maalum lilipitishwa kwa pamoja na wamiliki/wanahisa wa kampuni la kufunga kampuni kwani haijafanya shughuli zake.

Ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni, wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya siku 7 za taarifa hii.

Karimjee Attorneys
P.O. Box 76421
Dar es Salaam

157557

## HATI YA KIAPO

Mimi **JOYCE PETER MSUMBA,** umri 57, kabila MNYASA, dini MKRISTO, mkazi wa **KIJICHI, ILALA, DAR ES SALAAM.**

Nikiwa na akili timamu na bila kushawishiwa wala kulazimishwa na mtu yeyote naapa kwamba mimi ndiye mwenye jina tajwa hapo juu.

- Kwamba mimi nimepotelewa na OFFER iliyotolewa na Manispaa ya TEMEKE ya eneo la **GEZA ULOLE, lenye BLOCK 18, PLOT** 201 ukubwa wa mita 593 kikiwa na jina la **JOYCE PETER MSUMBA** ambapo nilipoteza mwezi wa 01/2020.
- Kwa kiapo hiki ninaomba Idara/Wizara/Ofisi husika itambue hivyo na iweze kunipatia huduma ninayostahili kupewa.
- Natoa tamko hili nikijua kuwa yote niliyoeleza hapo juu ni ukweli tupu na endapo itakuwa kinyume na kiapo hiki hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu mimi mtoa kiapo.

KIAPO HIKI KIMESAINIWA
MBELE YA ...
ANWANI ...
TAREHE 15/5/2020
CHEO ...
SAHIHI ...

SAHIHI YA MTOA KIAPO

157555

## IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA AT DODOMA PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.36. 2020

In the matter of the Estate of the **LATE HEZRON JOSEPH FUGUTILO** of Miyuji within Dodoma city

And

In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by YONA PETER FUGUTILO

**GENERAL CITATION**

(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 10/06/2020.

Dated at Dodoma this 27TH day of May 2020

RESIDENT MAGISTRATE
...............................................
DODOMA

157546

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA.

WADHAMINI BAKWATA KUTOKA MANISPAA YA SHINYANGA. WANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YAO YA KIWANJA NAMBA 693 KITALU "U" MWASELE MANISPAA YA SHINYANGA AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2020 MAENEO YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA WADHAMINI BAKWATA KWA SIMU NAMBA 0756-236835.

RB NAMBA SHY/RB/2020,
CONTROL NAMBA 991081269637.

157552

## JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo CHAMWINO MJINI

Usimamizi wa mirathi NA. 40/2020

Ombi la **ZENA AHMAMED KIMBUNGA** kuwa msimamizi wa mirathi marehemu **AHMED ABDALLAH KIMBUGA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnano tarehe 28-05-2020 kabla ya muombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Tarehe 12/05/2020

157547

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AYOUB ABDULRAHIM OMAR** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TRAILER YENYE NAMBA ZA USAJILI T498 BGU YENYE CHASSIS NO AMT -011015-10

KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
KAH/TR/RB/181/020

157745

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Anaitwa **STIGMATINE FATHERS CATHOLIC MISSION-MSOLWA** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 205 BDT aina yake **TOYOTA LANDCRUISER VX** yenye ingine namba **1HD0036894** na chasis namba **HDJ810013582.**

Kwa yeyote atakeiona anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:
MOR/MOR/RB/406155/2020.

157544

## JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Namba 71/2020**

**Ombi la JOSEPHINE WALLACE NICHOLAUS kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu WALLACE NICHOLAUS SACKEY**

**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 26/06/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .**

**Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.**

**Tarehe 26/05/2020.**

157543

NJOO

UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI

NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# ‘Vikundi rejesheni mikopo h/shauri’

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

VIKUNDI vilivyopata mikopo kutoka halmashauri na taasisi nyingine za kifedha vimeshauriwa kujenga uaminifu katika marejesho ili na wengine waweze kunufaika na fedha hizo.

Hayo yamebainika jana katika hafla ya kukabidhi hundi za mikopo awamu ya nne kwa baadhi ya vikundi vya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema benki hiyo ilikabidhiwa jukumu la kutoa elimu kwa vikundi pamoja na kuwafungulia akaunti, jambo ambalo wamelifanya kwa makini na vikundi vyote walifanikiwa kupata fursa hiyo.

“Mbali ya elimu ya fedha, NMB tunashirikiana na halmashauri hii kwa kutoa misaada mingine kwenye jamii hasa sekta ya elimu, afya na kwenye majanga mbalimbali,” alisema Mlozi.

Alisema benki hiyo imeendelea kutenga asilimia moja ya faida yake kila mwaka kurudisha kwenye jamii ikiwa ni juhudi za kuunga mkono Serikali ya Rais John Magufuli.

Mkurungenzi wa Halmashauri ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alisema jumla ya fedha zilizokopeshwa kwenye vikundi ni zaidi ya Sh. milioni 244.6 kutoka mapato yake ya ndani.

“Walionufaika ni wananchi 1,412 ndani ya halmashauri hii, wakiwamo wanawake 1,074 vijana 372 na walemavu 40. Halmashauri hii haidaiwi, imeshalipa madeni yote yakiwamo mikopo benki na makandarasi waliofanyakazi ya eneo hili.”

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zacharia Chaula, alivitaka vikundi vilivyopata fursa ya kupewa mikopo kutoka mfuko wa halmashauri kuhakikisha wanarejesha kwa wakati ili wengine waweze kufaidika na mikopo hiyo.

Alisema: “lengo la serikali kutoa mikopo hiyo kupitia halmashauri ni kuwajengea uwezo wa kiuchumi makundi maalumu yaliyoorodheshwa kisheria katika mikopo hiyo.”

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Simanjiro, Sendeu Laizer, alimshukuru Mkurungenzi wa Halmashauri hiyo na baraza la madiwani kwa kuhakikisha anatenga fedha hizo kwa kuwahudumia makundi maalumu.

Laizer aliishukuru benki ya NMB kwa kuwajengea makundi hayo uwezo wa elimu ya kifedha.

# Wabunge waja juu mifuko kuchelewesha pensheni

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wamechukizwa na kitendo cha mifuko ya hifadhi ya jamii kuchelewesha malipo ya pensheni kwa wastaafu, hususani walimu na wauguzi.

Wamesema idadi kubwa ya watumishi wanaojaa katika ofisi za mifuko ya hifadhi ya jamii wakifuatilia mafao yao ni walimu na wauguzi, ambao wamekuwa wakifuatilia kwa miaka mingi bila ya mafanikio.

Vilevile, wameitaka serikali kuhakikisha posho za madiwani zinalipwa kwa wakati kwani wengi wamekuwa wakikopwa jambo ambalo siyo sawa kisheria.

Hivyo, wameitaka serikali kuwa na mkakati wa kuhakikisha mifuko hiyo inaandaa malipo ya wastaafu mapema ili kuondoa usumbufu wa ufuatiliaji, pamoja na madiwani kulipwa posho kwa wakati.

Wakichangia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), kuhusu taarifa za ukaguzi za CAG kwa hesabu zilizokaguliwa za serikali za mitaa kwa mwaka 2018/19, wabunge hao walisema wastaafu wengi wanaangaika kufuatilia mafao yao kwa miaka mingi.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Rita Kabati, alisema mkoani Iringa kuna baadhi ya walimu tangu mwaka 2017 wanafuatilia mafao yao bila ya mafanikio.

Alisema walimu serikali inapaswa kuweka utaratibu mzuri wa maandalizi kwa wastaafu ili kuwaondolea usumbufu wa kufuatilia mara kwa mara.

“Serikali iweke data vizuri, kama mwakani idadi fulani wanastaafu basi waandaliwe fedha zao mapema, siyo vizuri kwa mtumishi wa serikali aliyetumikia kwa moyo wote miaka yote alafu aanze kuhangaika kufuatilia mafao yake,” alisema Kabati na kuongeza:

“Inaumiza sana, walimu, wauguzi hawalipwi kwa wakati, wanaangaika miaka miwili hadi minne, wakifuatilia wanapewa majibu mabaya,” alisema Kabati.

Kuhusu posho za madiwani, Kabati alisema: “Madiwani wamekuwa wakicheleweshewa posho zao, tunajua hawa watu hawana mishahara, sasa kuwacheleweshea posho zao ni kuwaweka katika wakati mgumu. Wapewe kwa wakati ili waendelee kutumikia kwa moyo.”

Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Susan Lyimo, alisema kuna watumishi wengi wanaangaika kufuatilia mafao yao pindi wanapostaafu.


Alisema kada za ualimu, madaktari wamekuwa wakihangaika kwa miaka mitatu hadi minne wakifuatilia mafao yao.

“Halmashauri nyingi hazipeleki makato ya wafanyakazi wake kwa wakati, hali inayosababisha pindi wanapostaafu kuanza kuhangaika. Ukienda katika mifuko ya hifadhi ya jamii idadi kubwa ya watu waliojaa ni walimu na wauguzi,” alisema Lyimo.

Kuhusu posho za madiwani, Lyimo alisema: “Madiwani wanafanya kazi usiku na mchana, wengi wanakopwa posho zao, naiomba serikali iwalipe kwa wakati kabla ya mabaraza kuvunjwa.”

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Aisha Rose Matembe, alisema madiwani katika halmashauri nyingine wamekuwa wakinyimwa posho zao na kusababisha wao kufanya kazi katika wakati mgumu.

Naye Mbunge wa Ukerewe, Joseph Mkundi (CCM), alisema kuna watumishi




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 244.6 Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zacharia Chaula (kulia), kwa ajili ya halmashauri hiyo kukabidhi mikopo kwa baadhi ya vikundi vya walemavu, wanawake na vijana. Benki ya NMB ilikabidhiwa jukumu la kutoa elimu ya kifedha kwa vikundi hivyo kabla ya kupewa mikopo hiyo, wengine katika picha katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Simanjiro, Yefred Myenzi (wa pili kulia) na Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Sendeu Laizer (wa pili kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**

# ‘Hatua zichukuliwe walimu watoro’

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

BAADHI ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga mkoani Pwani, wameomba Ofisi ya Mkurugenzi wa wilaya hiyo, kuchukua hatua dhidi ya walimu wa shule za msingi na sekondari ambao wamekuwa wakitoroka muda wa masomo.

Mbali na walimu hao kutoroka wakati masomo yakiendelea, pia wameomba walimu ambao wanafundisha shule za vijijini huku wanaishi mijini nao wachukuliwe hatua.

Juma Maghaila, Diwani wa Panzuo, aliibua hoja hiyo wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani Mkuranga.

Alisema walimu wa Shule ya Sekondari Panzuo wanalalamikiwa na wazazi na wanafunzi kwa kutoroka muda ambao vipindi vinaendelea.

Sultan Chechen, Diwani wa Njia Nne, alisema baadhi ya walimu wanaofundisha katika kata hiyo,wamekuwa wakiishi mjini badala ya vijijini ziliko shule walizopangwa kufanya kazi.

“Tunaomba sheria ichukuliwe kwa hao walimu ambao wanakaa mjini badala ya kukaa katika vituo vyao vya kazi,” alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Juma Abeid, alisema tayari walishachukua hatua kwa waratibu wa elimu wasio na sifa ambao waliwahamisha na kuwapeleka maeneo mengine.

Kuhusu walimu wasiofika shuleni wakati nyumba zao zipo, alisema walimu wa aina hiyo waliishawahamisha na kuwapeleka shule zingine.

# WERNER KUMRITHI MARTINEZ INTER



**MILAN,** Italia

KAMA Lautaro Martinez atakwenda Barcelona, Inter Milan inaweza kumsajili Timo Werner kama mbadala wake wakati Liverpool ikiwa imejitoa kwenye mbio za kuwania saini ya nyota huyo wa RB Leipzig, kwa mujibu wa gazeti la Corriere dello Sport.

Martinez na Werner ni washambuliaji wawili ambao wamekuwa wakihusishwa na uhamisho kuelekea mwishoni mwa msimu huu, baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia pale Inter na RB Leipzig.

Na Werner anaweza kwenda kuvaa viatu vya Martinez kwenye dimba la San Siro kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina ataondoka.

Werner ndiye anayeonekana kuwa chaguo la kwanza la kumrithi Martinez pale Inter kwa sababu klabu hiyo inaona kuna uwezekano mkubwa wa yeye kujiunga na Barcelona.

Werner kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa Liverpool, lakini gazeti la Mirror limeripoti vinara hao wa Ligi Kuu England wamejitoa kwenye mazungumzo na hawapo tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 50 ambacho zipo kwenye kipengele cha mkataba wake kama akitakiwa na timu nyingine.

Wakati huo huo, gazeti la AS limeripoti kwamba, Philippe Coutinho anaweza kuwa sehemu ya ofa ya Barca ili kumpata Martinez, kwani Inter imesema inataka euro milioni 111 kwa ajili ya kumwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

# Kulusevski afunguka kuhusu De Bruyne

**TURIN,** Italia

DEJAN Kulusevski aliyesajiliwa na Juventus ana matumaini kuwa kwenye kiwango bora zaidi kama nyota wa Manchester City, Kevin De Bruyne.

Kulusevski mwenye umri wa miaka 20, alinunuliwa na Juve kwa euro milioni 35 Januari kabla ya kurudishwa Parma kwa mkopo kumalizia kipindi cha msimu kilichobaki.

Straika huyo wa Sweden amesema amemwangalia kwa karibu sana De Bruyne na ana matumaini ya kumwiga nyota huyo wa Ubelgiji.

"Yeye ni mmoja wa wachezaji watano wa juu duniani," amesema Kulusevski akiiambia Sky Sport.

"Najifunza mengi kwa sababu yeye ni mchezaji wa aina yake na kwa sababu nataka kuwa kama yeye, lakini pia ni imara.

"Moja ya tabia yangu ni kuangalia mechi nyingi, kwa sababu najifunza mengi kutoka kwa wachezaji wenzangu."


Kulusevski alikuwa pia anahusishwa na kutakiwa Inter Milan kabla ya kusajiliwa Juventus.

Mchezaji huyo wa zamani wa Atalanta amesema Kocha wa Juve, Maurizio Sarri ilikuwa moja ya sababu kubwa ya yeye kuchagua kujiunga na mabingwa hao wa Serie A.

"Moja ya sababu kwanini nilichagua Bianconeri ilikuwa ni Sarri," amesema Kulusevski.

"Nafikiri naweza kufanya vizuri na kujifunza mengi kwake. Nilitazama mechi zake zote wakati akiwa Chelsea."





# *Cavani ashauriwa kutua Atletico*

**MADRID,** Hispania

EDINSON Cavani anaweza kutengeneza 'upatina' mzuri zaidi na Romelu Lukaku pale Inter Milan, lakini anaweza "kuwa na muda wa kufurahia zaidi" kama akihamia Atletico Madrid, amesema mchezaji mwenzake wa zamani kule Napoli, Andrea Dossena.

Mfungaji huyo wa wakati wote wa Paris Saint-Germain, Cavani atamaliza mkataba wake mwishoni mwa Juni na amekuwa akihusishwa kutua Inter na Atletico Madrid, ambako alitajwa zaidi katika dirisha dogo la Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 alitumia misimu miwili kule Napoli kati ya mwaka 2010 na 2013, akishinda Coppa Italia msimu wa 2011-12 akiwa na Dossena.

Mchezaji wa zamani wa Italia, Dossena haamini kama huu ni muda wa Cavani kutundika daruga na anahisi anaweza kuwa na mafanikio akienda Inter au Atletico.

Dosseana ameiambia Stats Perform News: "Nakumbuka kiwango chake cha kuvutia, na njaa yake ya mafanikio. Ni wachezaji wachache wenye ari kama yake. Amekuwa na malengo ya kutengeneza rekodi kwa rekodi na hilo ni jambo la kuvutia.

"Kwa uhakika kabisa hatakiwi kufikiria kuhusu kustaafu. Ana machaguo mawili; kwenda Atletico Madrid na Inter. "Bado ana nafasi kubwa ya kufanya vizuri kwenye soka na nina uhakika atakuwa na mafanikio zaidi akiendelea kucheza."

HABARI MICHEZO

# Mourinho: Spurs haitumii fedha nyingi kusajili

**LONDON,** England

JOSE Mourinho ametabiri kuchelewa kufunguliwa kwa dirisha la usajili kwa klabu za Ligi Kuu England na anatarajiwa kutakuwa na uangalifu mkubwa wa matumizi ya fedha.

Tottenham wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, na mara ligi hiyo itakaporejea baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, mashabiki watatarajia kuiona imeimarika.

Mourinho amesema wachezaji wapo tayari kurudi dimbani, lakini alishindwa kusema zaidi kuhusu usajili wa Tottenham Hotspur wakati dirisha litakapofunguliwa.

"Swali la kwanza ni kwamba, lini dirisha la usajili litafunguliwa?" Amesema Mourinho akiiambia Sky Sports.

"Sidhani kama itakuwa Julai au Agosti kama ilivyozoeleka, itakwenda mbali ya hapo.

"Ni kawaida tutakuwa na soko tofauti kabisa, sioni kama dunia ya soka ipo tayari kufanya usajili mkubwa kama ilivyozoeleka.

"Ningependa klabu yangu kuwa kama ninavyojua ilivyo, yenye uwiano na sio kutumia fedha fedha nyingi.



# BARCELONA YAPEWA MASHARTI KWA LAUTARO




**BARCELONA,** Hispania

MKURUGENZI wa Michezo wa Inter Milan, Piero Ausilio, amesema Lautaro Martinez hatauzwa Barcelona isipokuwa klabu hiyo ya LaLiga ikikubali kulipa fedha iliyopo kwenye kipengele cha mkataba wake cha kumwachia.

Nyota huyo wa Argentina, Martinez kwa muda sasa amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda kule Camp Nou akichukuliwa kama mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez, lakini dili hilo linaonekana kuwa gumu.

Barca walikuwa wakihangaika kufikia ada yake kabla ya mlipuko wa virusi vya corona na wameripotiwa wanajiandaa kuuza wachezaji kadhaa na kutoa ofa wengine ikiwa sehemu ya kukamilisha dili hilo.

Arturo Vidal, Nelson Semedo, Samuel Umtiti na Ivan Rakitic wametajwa huenda wakawa sehemu ya uwezekano wa kufanikisha dili hilo la kumpata mshambuliaji wa zamani wa Racing.

Hata hivyo, Inter imeweka wazi klabu yoyote inayomtaka Martinez itatakiwa kulipa kiasi chote cha euro milioni 111 iliyopo kwenye mkataba wake, na inatakiwa kulipwa kwa wakati mmoja.

Ausilio ameiambia Sky Sport: "Lautaro Martinez hauzwi. Barcelona waliwasiliana na sisi, tuna mahusiano nao mazuri, lakini tuliwaambia hatutamuuza Lautaro.

"Kama wanamtaka, Barca lazima ilipe kiasi chote kilichopo kwenye mkataba wake.

# *Napoli hatarini kumpoteza Koulibaly*

**NAPLES,** Italia

NAPOLI wanaweza kulazimika kumuuza Kalidou Koulibaly kama hawatafuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Andrea Dossena ameonya.

Ligi Kuu Italia bado haijaanza tena tangu iliposimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, na iliwaacha Napoli wakiwa nafasi ya sita na kupitwa pointi tisa na Atalanta iliyopo nafasi ya nne.

Kabla ya msimu huo kusimama, kocha wake Gennaro Gattuso alikuwa anaanza kujaribu kuinyanyua baada ya kuchukua mikoba ya Carlo Ancelotti, Desemba mwaka jana.

Dossena, ambaye aliichezea Napoli kati ya mwaka 2010 na 2013, anahofia klabu inaweza kuwapoteza wachezaji wake muhimu kama haitaweza kufuzu kwenye mashindano hayo ya Ulaya msimu ujao, ikiwa imefika hatua ya 16 kabla ya msimu kusimama.

Na ana uhakika Koulibaly ana uwezekano mkubwa wa kuondoka, kwani mlinzi huyo wa kati amekuwa akiwaniwa na Liverpool na Manchester United.

"Kupata pointi tisa ili kuipiku Atalanta ni changamoto, hivyo Napoli inaweza isifuzu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na watalazimika kuuza baadhi ya wachezaji wake," amesema Dossena akiiambia Stats Perform News.

"Wachezaji wawili ambao wana thamani zaidi ni Fabian Ruiz na Koulibaly; hao wana nafasi kubwa zaidi ya kuondoka."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MADRID YAENDELEA KUMWINDA POGBA

●●● Yatangaza kutoa wachezaji wake watano ili kufanikisha usajili wa Mfaransa huyo...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inajiandaa kuwatoa wachezaji wake wanne akiwamo, James Rodriguez na Martin Odegaard kujiunga na Manchester United ili kufanikisha mchakato wa kumsajili kiungo, Paul Pogba.

**Kocha wa Madrid, Zinedine Zidane, amekuwa akimwinda kwa muda mrefu mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka jana, Mfaransa Pogba, ambaye amekosa mechi kadhaa msimu huu kutokana na kusumbuliwa na maumivu ya kifundo cha mguu.**

Huku Madrid ikiendelea kupambana kuwania saini ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27, vigogo hao wa Hispania wanatajwa kuwa tayari kuwatoa Lucas Vazquez na Brahim Diaz kama sehemu ya usajili huo, gazeti la The Sun limeandika, ingawa United inasisita mchezaji huyo hauzwi.

Taarifa zinaeleza kuwa Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer anajiandaa kumrejesha Pogba katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo wakati mechi za Ligi Kuu England zitakaporejea tena hivi karibuni.

Solskjaer anataka kuwapanga katika safu ya kiungo cha kati, Pogba na Bruno Fernandes ambaye alitua United kwenye usajili wa dirisha dogo la Januari, baada ya nyota hao wawili kufanya mazoezi wiki hii.

Pogba amecheza mechi mbili tu tangu Septemba mwaka jana, na hajacheza mchezo wowote kuanzia Desemba 26, lakini ameutumia muda huu ambao soka lilisimama kufuatia kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona kujifua na kuimarisha kiwango chake.

Inaelezwa Madrid inajipanga kwa namna yoyote kuhakikisha inamnasa mchezaji huyo katika majira ya joto, lakini kutokana na 'kuyumba' kiuchumi baada ya janga la corona, vigogo hao wa LaLiga wameandaa kutoa wachezaji wake ili kusaidia usajili huo.

Rodriguez, ambaye alisajiliwa kutoka Monaco na baada ya kufanya vizuri kwenye fainali za Kombe la Dunia mwaka 2014, ameshindwa kung'ara katika kikosi cha Bernabeu, kwa sasa alikuwa kwa mkopo wa miaka miwili Bayern Munich kuanzia msimu wa 2017/19.

Wakati Odegaard aliyesajiliwa akiwa na umri wa miaka 16, Januari kwa 2015, amecheza mechi mbili tu katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo na sasa yuko kwa mkopo kwenye timu yao ya Real Sociedad, baada ya huko nyuma kuzitumikia SC Heerenveen na Vitesse Arnhem.

Kiungo mshambuliaji, Vazquez yeye alitua Madrid akitokea kwenye akademi yao huku Diaz alisajiliwa kutoka Manchester City mapema Januari mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### KLOPP AMTAKA TRAORE

LIVERPOOL imesema inataka kumsajili winga wa Wolves, Adama Traore ambaye ana umri wa miaka 24, na tayari kocha wa timu hiyo, Jurgen Klopp ameanza mazungumzo binafsi na Mhispania huyo. ***(Todo-Fichajes - in Spanish)***

### IGHALO AITAKA UNITED

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Odion Ighalo (30), amewasilisha maombi rasmi ya kutaka kuendeleza mkataba wake wa mkopo katika klabu ya Manchester United kwa timu yake 'mama' ya Shanghai Shenhua ya China. ***(Manchester Evening News)***

### LUIZ NJIA PANDA

MKATABA wa mkopo wa beki wa kati, David Luiz ndani ya kikosi cha Arsenal unatarajiwa kumalizika mwezi ujao, huku kukiwa hakuna mazungumzo yoyote ya kuongeza mkataba mwingine yaliyofanywa kati ya Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 33 na klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

### LIVERPOOL YAWEKA NGUMU

LIVERPOOL imesema haiko tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 50 kilichowekwa katika mkataba ili kumnunua straika wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (24), na imeeleza rasmi leo wamewasilisha ofa ya pauni milioni 30 kwenye dirisha la usajili lilifunguliwa. ***(Mirror)***

### TAGLIAFICO ANUKIA CHELSEA

BEKI wa kushoto wa Ajax na Timu ya Taifa ya Argentina, Nicolas Tagliafico, ambaye ana umri wa miaka 27, anatarajia kujiunga na Chelsea kwa dau la pauni milioni 22.4. ***(Telegraph - subscription required)***

### FRASER AKARIBIA SPURS

MABOSI wa Tottenham wanajiimarisha kuzipiku klabu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu England ili kunasa saini ya winga wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Scotland, Ryan Fraser ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### MANQUILLO AIWAZA LA LIGA

BEKI wa Newcastle Mhispania Javier Manquillo (26), amesema anataka kujiunga na klabu yoyote ya La Liga baada ya mkataba wake kumalizika mwezi ujao ili kupata nafasi ya kurejea nyumbani kwao. ***(Newcastle Chronicle)***

### UNITED, MADRID VITANI

MANCHESTER United na Real Madrid zote zinatajwa kuwania saini ya kiungo wa Rennes na Timu ya Taifa ya vijana ya Ufaransa ya umri chini ya miaka 21 (U-21), Eduardo Camavinga ambaye ana miaka 17. ***(Metro)***

### MOURINHO AFUNGUKA

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amesema klabu za Ligi Kuu hazitarajiwi kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kusajili kwenye dirisha lijalo litakalofunguliwa. ***(Sky Sports)***

### SILVA MAMBO BADO

BEKI wa PSG, Thiago Silva ambaye atakuwa mchezaji huru katika majira ya joto ametajwa kuwindwa na klabu mbalimbali ikiwamo AC Milan. ***(Calciomercato)***

HABARI MICHEZO

## Azam FC kurudi na nguvu mpya

**Na Shufaa Lyimo**

KIUNGO mkongwe wa Azam FC, Frank Damayo, amesema amefarijika kuona wachezaji wameanza mazoezi ya pamoja baada ya Rais Dk. John Pombe Magufuli kutangaza kufungua michezo hapa nchini.

Wachezaji walisimama kucheza ligi na kufanya mazoezi ya pamoja tangu Machi 17, mwaka huu ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Akizungumza na gazeti hili jana, Damayo alisema wamejipanga kuimarisha ushirikiano ili kutimiza malengo ya klabu yao ya msimu huu unaoelekea ukingoni.

"Nimefarijika kukutana na wachezaji wenzangu mazoezini baada ya kutokuonana kwa muda mrefu, mpira ndio kazi yetu, tulikumbuka sana kucheza, tumerudi na nguvu mpya," alisema Domayo.

Aliongeza kwa upande wake alikitumia vizuri kipindi cha mapumziko kwa kufanya mazoezi kama alivyoelekezwa na makocha wake kwa sababu alitaka kurejea akiwa fiti na imara kumalizia msimu.

"Tutaendeleza ushindani kwa lengo la kushika nafasi ya juu katika msimamo wa ligi, tunawashukuru mashabiki na tunaomba wazidi kutupa ushirikiano ili tutimize malengo tuliyonayo," Domayo alisema.

## Mbio za magari zawaza mashabiki

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Mbio za Magari Tanzania (AAT), kimesema kimekamilisha kuandaa programu zake na kiko tayari kukutana na viongozi wa Baraza la Michezo Nchini (BMT), ili kujadiliana na kupanga mikakati.

BMT imevitaka vyama vyote vya michezo kuwasilisha programu zake kwa ajili ya kutoa mwongozo wa utekelezaji wake katika kipindi hiki cha janga la corona.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Uhusiano wa AAT, Athuman Khamis, alisema wanatarajia kikao hicho kitasaidia kufanyika kwa mashindano yao baada ya viongozi wa chama kukutana na kujadiliana kwanza.

"Mchezo wetu unakusanya watu wengi, lazima tukubaliane na wito huo wa serikali juu ya kupeleka programu na mikakati yetu, hii itatusaidia kupata ufafanuzi juu ya kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya corona," Khamisi alisema.

Aliongeza endapo mchezo huo utarejea bila ya kuhusisha mashabiki, kwao itakuwa ni changamoto na hasa kwa upande wa kiuchumi.

"Tunasubiri agizo la serikali, suala la kutokuwa mashabiki kwetu ni mtihani, sisi tunapata pesa kwa wale wanaokuja kushuhudia mashindano yetu ili kusaidia chama na shughuli nyingine, kiuchumi tutayumba," aliongeza kiongozi huyo.

# KAGERA SUGAR KAMILI KUTOA 'DOZI' LIGI KUU

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema kikosi chake kimeshaanza mazoezi na kiko tayari kushuka dimbani kumaliza mechi za msimu wa mwaka 2019/20 wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mtindo wowote.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Maxime alisema kikosi chake kiko imara na wamejiandaa kupata ushindi kwenye mechi zilizobakia ili waendelee kubakia katika Ligi Kuu Bara.**

Maxime alisema wachezaji wote wako salama mkoani Kagera na benchi la ufundi linatekeleza programu za mazoezi bila ya changamoto yoyote.

"Sisi tuko tayari, tunasubiri kipenga tu, tumejiandaa kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika michezo iliyobakia, hilo ndilo tunalolifikiria," alisema Maxime.



Beki huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Taifa Stars, alisema jambo muhimu ni kukijenga imara kikosi kwa ajili ya kutafuta ushindi bila ya kujali watacheza kwa mtindo upi.

"Kikosi changu kipo fiti na kusaka ushindi kokote tutapocheza, kikubwa ni kuzingatia ushauri wa Wizara ya Afya juu ya kujikinga na ugonjwa wa corona," alisema Maxime.

Aliongeza wamefanya maandalizi bora na ana imani na wachezaji wake watafanya vizuri katika mechi hiyo bila kujali watacheza nyumbani au ugenini.

Kagera Sugar ambayo msimu uliopita ilinusurika kushuka daraja, ina pointi 41 na kwenye msimamo iko kwenye nafasi ya nane baada ya kushuka uwanjani mara 29.



Wachezaji wa Polisi Tanzania FC wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Bara zinazotarajiwa kurejea hivi karibuni kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi, Kilimanjaro. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Klabu Zanzibar zatakiwa kusubiri

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

BAADA ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutangaza kurejesha Ligi Kuu ya Visiwani humo, Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), limesema linasubiri mwongozo kutoka kwenye Wizara ya Michezo pamoja na Wizara ya Afya, ili kutangaza ratiba mpya.

ZFF imesema mwongozo huo ndio utasaidia kuzipa muda wa maandalizi timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa ZFF, Mohamed Ali Hilali, alisema ni mapema kutangaza ratiba ya Ligi Kuu mpaka pale watakapopewa mwongozo wa namna ya ligi hiyo itakavyorejea.

Hilali alisema timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar zinatakiwa kusubiri taarifa hiyo na wanazikumbusha kuendelea kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

"Serikali imeruhusu kuendelea na ligi, lakini tunaviomba vilabu kusubiri mwongozo kutoka wizarani ndio waanze mazoezi ya pamoja ya kujiandaa na ligi yetu, hii yote inatokana na kutokea kwa janga hili la corona," alisema Hilali.

Kiongozi huyo aliwataka wafanyakazi wa ZFF kurejea kazini ili kushiriki kikamilifu maandalizi ya ligi ambayo wakati wowote itaanza kuchezwa visiwani hapa.

Hata hivyo, hatima ya mashindano ya Kombe la FA, ambayo hutoa mwakilishi wa Zanzibar katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika bado haijajulikana.

# Michezo

Ijumaa Mei 29, 2020

Nipashe




Madrid yaendelea kumwinda Pogba UKURASA 22

KAZIKAZI..



Wachezaji wa Simba wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi zilizosalia za Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20 kwenye Uwanja wa Mo Arena juzi jioni. **PICHA: SIMBA SC**

# MSOLLA AIPELEKA YANGA HISPANIA

●●● Ni namna itakavyojiendesha kisasa baada ya 'ndoto' zake za mfumo wa mabadiliko...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI zoezi la kusaini mkataba wa kuelekea katika mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa Yanga linatarajiwa kufanyika kesho jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla, amesema anaiona njia ya mafanikio inakaribia kufunguka.

**Endapo Yanga itafanikiwa kubadilisha mfumo wa uendeshaji, itakuwa imeungana na watani zao, Simba ambao waliingia kwenye mabadiliko hayo tangu mwaka juzi.**

Akizungumza na gazeti hili jijini, Msolla, alisema anawaomba wanachama na mashabiki wa Yanga kudumisha umoja katika kipindi hiki cha mabadiliko ili malengo waliyokuwa nayo yakamilike.

Msolla alisema kuwa bila ya umoja kati ya viongozi, wanachama, mashabiki na wadhamini, hakuna jambo ambalo linaweza kufanikiwa kwenye mchakato huu.

"Moja ya dhamira yangu wakati nagombea uongozi ilikuwa ni suala la klabu, sasa nadhani ndoto hii inaelekea kukamilika, ombi langu kwa wanachama na wapenzi wa Yanga, tuungane na uongozi, wadhamini, twendeni pamoja, Yanga lazima ifanikiwe," alisema Msolla.

Aliongeza kuwa wakati bado mfumo huo haujafikiwa, tayari wachezaji mbalimbali wa kimataifa wameanza kuonyesha nia ya kuja kujiunga na Yanga na hii ni dalili nzuri kwa klabu yao.

"Hapa katika orodha yangu nina majina zaidi ya wachezaji 40 wa kimataifa ambao wako tayari kutua Yanga, lakini sisi kwa kushirikiana na wadhamini wetu tutafanya usajili wa makini kuelekea msimu mpya, naomba tutulie, mambo mazuri yanakuja," Msolla alisema.

Alisema wanachama wa klabu hiyo watarajie kuona matokeo chanya baada ya mfumo huo kuanza kufanya kazi.

Naye Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema mabadiliko hayo yatasaidia kuongeza thamani ya klabu yao. Nugaz alisema uzoefu wa wadau wao kutoka LaLiga ambao wamefanya kazi na klabu zaidi ya 40, unawajengea imani kuwa Yanga inaelekea kwenye mafanikio na itakayoweza kujiendesha yenyewe.

Mwanasheria mkongwe nchini, Alex Mgongolwa ambaye ni mwanachama wa Yanga, ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Mabadiliko.

## Mmachinga: 'Yes' Kagere ni mashine

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuitazama kasi ya mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere katika kupachika mabao, straika nyota wa zamani wa Yanga, Mohammed Hussein 'Mmachinga' amesema ana imani Mnyarwanda huyo anaweza kuvunja rekodi yake kwa kufunga mabao mengi msimu huu.

Mmachinga anashikilia rekodi ya kufunga mabao 26 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, huku mshambuliaji wa zamani wa Mtibwa Sugar, Abdallah Juma, alikaribia rekodi hiyo baada ya kufunga magoli 25 katika msimu wa mwaka 2014/15.

Kagere anaongoza katika orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu akiwa na mabao 19 akifuatiwa na Reliants Lusajo wa Namuungo, Yusuph Mhilu (Kagera Sugar) na Paul Nonga wa Lipuli, ambao kila mmoja ana magoli 11.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mmachinga alisema uwezo wa mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Rwanda ni mkubwa kwa sababu anajituma zaidi anapokuwa uwanjani.

Mmachinga alisema sababu ya kuamini Kagere ana nafasi ya kuvunja rekodi yake iliyodumu kwa muda mrefu ni baada ya kusikia mikakati iliyowekwa na benchi la ufundi la mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo linaloongozwa na Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

"Mbali na mikakati ya benchi la ufundi la Simba katika kuhakikisha anafikia rekodi, sitaona ajabu Kagere kuvunja rekodi yangu iliyodumu kwa muda mrefu kwa sababu ni mtu wa kazi," alisema Mmachinga.

"Ni mchezaji ambaye anajituma, ukiangalia huu ni msimu wa pili sasa anachukua tuzo ya ufungaji bora, kwa kasi yake nina imani ana uwezo wa kufunga mabao saba au zaidi katika michezo 10 iliyobakia," Mmachinga alisema.

Aliongeza atafurahi kuona rekodi yake inafikiwa na kuvunjwa, lakini furaha ingeongezeka zaidi kama mchezaji mzawa ndio 'angepokea kijiti' hicho kutoka kwake.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042